**26 AGOSTI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

_________

# MAJADILIANO YA BUNGE

_________

## MKUTANO WA NNE

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 26 Agosti, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### TAMKO LA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Tamko la Ahadi. Nitawaongoza.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walisoma Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**26 AGOSTI, 2026**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali. Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Kwa niaba, Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 1

**Kukamilisha Ujenzi wa Vyumba vya Maabara Katika Shule ya Sekondari Msakwalo - Chemba**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. AISHA M. MDUYAH** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa vyumba viwili vya maabara katika Shule ya Sekondari Msakwalo iliyopo Kata ya Ovada, Wilayani Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Profesa Shemdoe, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012, ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara katika Shule ya Sekondari Msakwalo ulianza kwa nguvu za wananchi, ambapo ujenzi huo ulifikia 45%. Aidha, mwaka 2022, Serikali iliunga mkono juhudi za wananchi kwa kupeleka shilingi milioni 35, kwa ajili ya kukamilisha chumba kimoja cha maabara ambacho kilikamilika na kinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2026/2027 Serikali, kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, imetenga shilingi milioni 30, kwa ajili ya kukamilisha chumba kimoja cha maabara katika Shule ya Sekondari Msakwalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya shule zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, ikiwemo Shule ya Sekondari Msakwalo, kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri kwanza ninaipongeza Wizara yako kwa kazi kubwa mnayoifanya na jitihada za Serikali yetu, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata hivyo, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza; kwenye jibu lako la msingi umezungumzia halmashauri kutenga shilingi milioni 30, kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya maabara na utakubaliana na mimi kwamba, halmashauri nyingi bado vipato vyao ni vidogo. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo yote ambayo wananchi wameanza ujenzi kwa maabara wanaweza kukamilishiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mbali na changamoto za maabara, kwenye shule nyingi za sekondari kumekuwa na upungufu wa mabweni, hasa katika Jimbo la Bunda Mjini. Ukienda pale Shule ya Bunda Sekondari, ambayo inafanya vizuri, tena imekuwa namba moja kwenye Mkoa wa Mara, kuna upungufu wa mabweni na maeneo mengine katika Jimbo la Bunda Mjini. Ni lini sasa Serikali itahakikisha inajenga mabweni, ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wetu na ufaulu unaongezeka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza pia, Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kuuliza swali la nyongeza, kwa niaba ya Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah,

ambaye anajitahidi sana kuwasemea wananchi wa Mkoa wa Dodoma, ikiwemo pia Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli halmashauri zetu nyingi zina vipato vidogo, lakini utakubaliana na mimi kwamba, hizi halmashauri tumezigawa kwenye makundi kwa namna ya kupeleka fedha za maendeleo. Kuna ambazo zinatakiwa kupeleka 70%, kuna ambazo zinatakiwa kupeleka 40%, pia, kuna ambazo zinatakiwa kupeleka 20%. Kwa mantiki hiyo, tulivyokuwa tunapitisha bajeti tuliangalia Halmashauri ya Chemba inatakiwa kupeleka asilimia ngapi, ili kufanya miradi ya maendeleo ionekane. Ndipo hapo sasa ambapo pamesababisha Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kupeleka fedha hizo, shilingi milioni 30, kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea tu kusema kwamba, Serikali inaendelea kutafuta fedha, ili kuweza kukamilisha maabara na miundombinu mingine yote, ambayo imeanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili la nyongeza, Mheshimiwa Ester Bulaya umeuliza suala la mabweni na umezungumzia sana kwenye Halmashauri yako ya Bunda. Hapo, umechukua *advantage* ya Chemba, lakini umeenda Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, Waheshimiwa Wabunge wote hapa wakisimama wanaulizia suala la mabweni kwa sababu, ni ukweli usiopingika kwamba, tunahitaji kuwaweka wanafunzi karibu, ili waweze kupata elimu yao kwa ukaribu na usalama zaidi. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kutafuta fedha, ili tuone namna ya kujenga mabweni, hasa kwenye zile shule ambazo ziko mbali na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita iko tayari na inafanya kazi hii ya kutafuta fedha, ili tuweze kujenga mabweni kwenye shule zetu hizi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Shule ya Sekondari Mswakalo ni shule pekee inayofanya vizuri ndani ya Wilaya ya Chemba na Mheshimiwa Waziri hilo unalijua, lakini watoto wetu wanashindwa kukamilisha ndoto zao. Kwa mfano, matokeo ya safari hii tuna *division one* na *two* peke yake, hatuna *three* wala *zero,* lakini watoto hawa wanashindwa kutimiza ndoto kwa kutokuwepo tu kwa hizo maabara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Halmashauri ya Wilaya ya Chemba mapato yetu unayajua, mnatakiwa kutuletea 70%. Hatuna uwezo wa kutenga fedha za ndani, kwa ajili ya ujenzi wa maabara au kukamilisha nguvu za wananchi. Wananchi wetu wameendelea kufanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba, wanatimiza ndoto za watoto wetu, kwa ajili ya kuja kuwa viongozi wa kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kauli ya Mheshimiwa Waziri, kwa ajili ya kutupatia hiyo shilingi milioni 30 nyingine ya pili, ili twende tukakamilishe majengo haya, watoto wetu waendelee kufanya vizuri na hatimaye tuweze kuandaa Taifa la kesho lenye weledi, utu, ubinadamu na uungwana wa Taifa lao, kwa ajili ya kuja kulitumikia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Kunti Majala, Mbunge wa Chemba, kwa kuwasemea sana Wananchi wake wa Chemba. Siyo hili la Shule ya Sekondari Msakwalo tu, lakini huwa anafanya mambo mengi kuhusu maendeleo ya Wananchi wa Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la shilingi milioni 30, namhakikishia Mheshimiwa Kunti kwamba, bajeti iliyopita tuliielekeza halmashauri ile kutokana na fedha ambazo wametenga, kwa ajili ya miradi ya maendeleo kupeleka fedha ile na tumepitisha hapa Bungeni kwamba, Halmashauri ya Chemba ipeleke shilingi milioni 30. Suala la kuongeza shilingi milioni 30 nyingine, Mheshimiwa Kunti Majala nakuhakikishia kwamba,

tutakapopata fedha mara moja tutaona namna ya kuzipeleka fedha hizo kwenye Shule hii ya Msakwalo, ili kukamilisha zile maabara zote mbili zilizobaki na wanafunzi wale waendelee kusoma kwa juhudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pongezi sana Shule ya Msakwalo kwa namna wanavyofanya vizuri kwenye masomo yao. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Shule ya Sekondari Matombo kuna mradi wa ujenzi wa bwalo la chakula, bweni la wasichana, pamoja na uzio. Sasa ni mwaka wa pili mradi huo umesimama. Je, ni lini Serikali itakwenda kuendelea na mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mfaume, kwa swali hili la nyongeza ambalo ameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli tunafahamu ujenzi huo umesimama, lakini nitapeleka timu mara moja iende ikaangalie shida ya pale ilikuwa ni nini na tuone namna ya kuweza kukwamua jambo hili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, ninaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya kazi kubwa ya kujenga shule katika Jimbo la Kalenga. Bahati mbaya shule zile za zamani kwa kweli, kutokana na uwezo wetu hazina maabara; zipo ambazo zina maabara

moja, nyingine mbili, wakati tunahitaji maabara angalau tatu, ili kutimiza ile haja ya wanafunzi kuweza kusoma masomo yote ya sayansi. Je, ni lini Serikali itatupa bajeti, ili tuweze kujenga hizo maabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Kiswaga kwa kuuliza swali la nyongeza. Swali hili hakuulizia, kwa ajili ya halmashauri yake pekee ama jimbo lake pekeyake, lakini ameliuliza kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya tathmini kuona ni maabara ngapi ambazo zinatakiwa kujengwa kwenye shule zetu za sekondari nchi nzima, ili kuwawezesha wanafunzi wetu kusoma masomo ya sayansi. Tutakapopata fedha tutahakikisha kwamba, tunapeleka angalau kwa kila jimbo na kwa kila halmashauri fedha hizo, ili tuweze kujenga maabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hapa wote watakuwa mashahidi kwamba, kuanzia mwezi wa tano hadi mwezi huu wa nane tumepeleka fedha, kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hasa kwenye masuala ya madarasa na shule. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo, ili tutakapopata fedha tuweze kuzipeleka huko, kwa ajili ya ujenzi wa maabara kwenye shule zetu hizi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa *Engineer* Kija Limbu Ntemi, Mbunge wa Katoro, sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Majimbo ya Katoro na Busanda kuwa Halmashauri**

**MHE. REGINA H. MIKENZE K.n.y. MHE. KIJA L. NTEMI** aliuliza:-

Je, hatua gani zinahitajika ili kupatiwa Halmashauri Jimbo la Katoro na Busanda, ambayo yamekidhi vigezo vya kuwa na halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa na Mamlaka za Wilaya, Sura 287 na Mamlaka za Miji, Sura 288, pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2025, ambao umeainisha vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa, ili kupandisha hadhi na kuanzisha maeneo mapya. Taratibu zinazopaswa kufuatwa ni kuwepo kwa kusudio la kuanzisha halmashauri mpya, ambalo linapaswa kujadiliwa na kupitishwa kuanzia ngazi ya Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* kisha maombi hayo kuwasilishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa na kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusudio la kupatiwa Halmashauri kwa Jimbo la Katoro na Jimbo la Busanda baada ya kutolewa Mwongozo wa Uanzishaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2025, bado halijawasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, hivyo mamlaka zinazohusika ziendelee na taratibu kwa kufuata Sheria na Miongozo iliyoainishwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina Mikenze, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini bado ninapenda kuuliza maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na adha kubwa wanayopitia wananchi wa Majimbo mawili ya Katoro na Busanda. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kufanya haraka

sana kuwapelekea halmashauri, ili kuweza kuwanusuru na adha hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa, katika Jimbo la Katoro tunalo jengo ambalo lipo tayari, kwa ajili ya halmashauri. Je, hatuoni kama linaweza kusaidia kuharakisha harakati hizo za kulipatia Jimbo la Katoro na Busanda halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, ambayo yameletwa kwa niaba ya Mheshimiwa *Engineer* Kija Limbu Ntemi, juu ya jambo hili. Wizara iko tayari kupokea, kujadili na kupeleka kwa uharaka maombi haya kwa mamlaka, kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, kutokana na mwongozo uliotolewa mwaka 2025, Halmashauri hii ilipelekewa mwongozo ule, ili waweze kuleta kwa kuzingatia vigezo vilivyotolewa. Vigezo hivi ni idadi ya watu, ili tuweze kuanzisha halmashauri mpya ni lazima tuwe na watu wasiopungua laki tano. Kwa Katoro kwa sasa ni kweli idadi ile imezidi, tuna watu zaidi ya milioni moja, kwa hiyo kigezo hiki wamekitimiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vigezo viwili vingine ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Geita inatakiwa ivitimize; cha kwanza ni ukubwa wa eneo na cha pili ni kujitegemea. Kwamba, ili halmashauri iweze kupewa kuwa halmashauri ni lazima iwe na uwezo wa kifedha wa kujitegemea usiopungua asilimia 50. Kwa leo hii Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina uwezo wa kujitegemea kwa asilimia 26 tu. Tumewapelekea mwongozo ule waweze pia kuleta, ili jambo hili tuweze kulifanyia kazi kwa uharaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza ni kuhusu uwepo wa utayari kwa kuwa na jengo ambalo lingeweza kutumika, kwa ajili ya kuanzisha halmashauri hii. Pindi watakapotimiza vigezo hivi tuna uhakika kwamba, Wizara yetu

italichukua jambo hili na kulifanyia kazi kwa haraka, ili na jengo lile baadaye liweze kutumika. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhael Lufungija, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Ninataka nipate majibu kwa Waziri. Jimbo la Ulyankulu liliahidiwa kuwa na Halmashauri yake ya Ulyankulu na ahadi hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Rais wetu Mstaafu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2010. Wananchi hawa kwa mahitaji makubwa, ikumbukwe mwaka 2010 hata uchaguzi waligoma, lakini Serikali iliahidi kuwapa halmashauri na mpaka sasa 2015 pia, iliahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kupata majibu. Je, ni lini Halmashauri ya Ulyankulu itakubaliwa kuanza kwa sababu, tayari vigezo vyote ambavyo Waziri amevieleza na kutimiza vikao tulikwishafanya; ninataka nipate majibu ya Serikali, ni lini sasa Halmashauri ya Ulyankulu itaanzishwa, ili kujibu hoja ya wananchi hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mbunge wa Ulyankulu kwa kuuliza swali lake la nyongeza kuhusu ni lini Serikali itaanzisha halmashauri kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, kuna mwongozo ambao umekwishatolewa, wa mwaka 2025. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge, tukitoka hapa nimpatie mwongozo ule, ili aurejeshe kwenye halmashauri mama na waweze kuanza mchakato huo, ambapo unaanzia kwenye halmashauri mama, unakwenda kwenye wilaya, kwenye vikao vya *DCC*, unakwenda kwenye mkoa kwenye vikao vya *RCC* na hatimaye ile taarifa inaletwa Wizarani kwetu, ili tuweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa

Mbunge tutakapotoka hapa tuonane, ili nimpatie mwongozo ule. Nitamwambia Katibu Mkuu na timu yake wapeleke mwongozo ule kwa Mkurugenzi, ili kazi yao iweze kuanza. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Halmashauri ya Bunda imeanzishwa mwaka 1980, ikatoka hapo mwaka 1995 ikagawanyika kuunda Jimbo la Mwibara, ambalo tayari lina halmashauri mpya. 2015 likapatikana Jimbo la Bunda Mjini, tayari lina Halmashauri imejengwa. Majengo yaliyokuwa ni ya Halmashauri ya Bunda yako wazi na sisi leo tunatembea tunaenda Kibara, kilometa 140. Je, ni lini watatturudisha kwenye majengo yetu na kuteua Mkurugenzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Getere kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye jimbo lake. Mheshimiwa Getere jambo hili tumelijadili sana, mimi na yeye. Tuko kwenye mpango wa kuona ni namna gani sasa tunaweza kutumia majengo yale yaliyo wazi, ili wananchi wanaozunguka kutoka Bunda wapite Bunda Mjini ndipo waende kwenye jimbo la Mheshimiwa Getere waweze kupata huduma kwa ukaribu. Kwa hiyo, tutaendelea kulijadili suala hili, mimi na yeye Mheshimiwa Getere, pamoja na wataalam wetu, ili tuone ni namna gani tunaweza kutatua jambo hili. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 3

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Katika Kata ya Mfereji**

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya cha Mfereji ikizingatiwa

kuwa, fedha za ujenzi wake zilitengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali alilolileta Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mfereji ina jumla ya wakazi 8,068 na ina vijiji vinne vya Komesha, Emurua, Idonyonado na Mfereji. Vijiji vya Mfereji na Idonyonado vina zahanati zinazotoa huduma. Aidha, Kijiji cha Emurua, ujenzi wa zahanati upo hatua ya ukamilishaji na Kijiji cha Komesha ujenzi upo hatua ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Serikali imetoa shilingi milioni 250, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya, Kata ya Sepeko, katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Ujenzi umehusisha jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje (*OPD*), jengo la maabara, choo cha nje na kichomea taka. Aidha, ujenzi umekamilika na kituo kimeanza kutoa huduma kuanzia mwezi Julai, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wakazi wa Kata ya Mfereji wanapata huduma za rufaa na dharura katika hospitali ya wilaya wakati Serikali ikiendelea kutenga fedha na kujenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati zitakazokidhi vigezo kote nchini, ikiwemo Kata ya Mfereji katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marirta, huna swali la nyongeza! Swali la nyongeza?

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umbali mrefu kutoka Kata ya Mfereji mpaka Hospitali ya Wilaya ya Monduli, ambapo

wananchi wetu ndipo wanapopata huduma kwa sasa. Je, Serikali ina dhamira gani mahususi ya kuhakikisha fedha zinatengwa, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Mfereji na kukamilika kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge kwa kuwasemea Wana-Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba, Kata ya Mfereji ni moja ya kata za kimkakati. Sisi, kama Wizara, tumekaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha tukiwaomba shilingi bilioni 23, ili tuweze kujenga vituo vya afya 94 kwenye halmashauri zetu zenye kata hizi ambazo ni za kimkakati, ikiwemo Kata ya Mfereji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pale ambapo fedha hizi zitatoka, tunawahakikishia Wana-Kata ya Mfereji kwamba, tutapeleka fedha hiyo, ili waanze kujenga kituo cha afya kwenye Kata ya Mfereji. Ninawasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni takribani mwaka mzima amezungumzia suala la kutoa fedha, kwa ajili ya kujenga vituo vya afya. Ndani ya Bunge hili kuna Wabunge waliopata fedha na kuna Wabunge hatujapata fedha hadi leo kiasi kwamba, wananchi hawatuelewi, nikiwemo mimi Kata ya Matamba, ndani ya Jimbo la Wilaya ya Makete.

Je, ni lini fedha zitatoka ili sisi Wabunge ambao hatujapata, tupate fedha hizi, ili siasa yetu majimboni iweze kutulia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na

namshukuru sana Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete, kwa kuuliza swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika kwamba, hizi *microphones* zote unazoona zimewaka sasahivi ni wale 94 ambao hawajapata fedha ile ya awamu ya kwanza tuliyopeleka kwenye Halmashauri zingine na kwenye majimbo mengine. Nakuhakikishia kwamba, mimi na Waziri wa Fedha tumekaa na tumekubaliana kwamba, *flow* ya fedha itakapokuwa nzuri tutapata fedha hizo, shilingi bilioni 23, ambazo tutazipeleka kwenye vituo hivi 94 mara moja, kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimuondoe shaka Mheshimiwa Festo Sanga kwamba, fedha ile itapatikana kwa sababu, ndiyo tumeanza tu mwaka; fedha hii ikipatikana tutaipeleka kwenye vituo hivyo 94, kikiwemo kituo alichokitaja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ado Shaibu, swali la nyongeza.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza swali langu la nyongeza; kwa kuwa, kwenye Mkutano wa Bunge uliopita niliomba Mwongozo wa Kiti cha Spika juu ya hatma ya vituo vya kimkakati. Na kwa sababu, sasa Mheshimiwa Waziri amesema msimamo wa Serikali ni kwamba, Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha wanafanya kazi kwa Pamoja, kuhakikisha fedha zinapatikana, ili kuwezesha kumalizika kwa vituo vile vyote vya kimkakati. Ninaomba kwanza niondoe sasa lile ombi langu la mwongozo kwa sababu, nimeupata vizuri kupitia kauli ya Waziri. Nawashukuru kwamba, kwenye kituo chetu nilichokiombea wakati ule, cha Nampungu, kimepelekewa fedha zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu. Mwaka 2010 Mheshimiwa Rais Magufuli, wakati wa kampeni, alitoa ahadi ya kujenga kituo cha afya katika Kata ya Namiungo, ambayo ina vijiji saba na ni kata kubwa sana yenye wakazi wengi...

**NAIBU SPIKA:** Ngoja kwanza Mheshimiwa. Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** ...ninauliza swali sasa. Ni lini ahadi hii itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge samahani. Umesema mwaka gani?

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, 2015.

**NAIBU SPIKA:** Hapo sawa, ulisema 2010. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ado Shaibu, kwanza kwa kuondoa mwongozo ule ambao alikuwa ameuleta Bungeni. Hii inaonesha ni namna gani Mheshimiwa Ado amekuwa mwenye busara sana kuona kwamba, hakuna haja ya kuendelea kujadili jambo hili kwa sababu, limepata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kata hii anayoitaja Mheshimiwa Ado ni moja ya kata ambazo zinatakiwa kupelekewa fedha, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya pale. Ni kweli tunafahamu kwamba, kata ile ina vijiji saba ambavyo vinategemea kupata huduma, kama tutajenga kituo cha afya pale. Kwa hiyo, namhakikishia tu Mheshimiwa Ado, na ninafahamu anafahamu uchapakazi tulionao kwenye Wizara yetu, tutahakikisha tunampelekea kituo hicho cha afya pindi tutakapopata fedha. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Swali langu linahusu kituo cha afya; mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ilituletea Bungeni mapendekezo ya kuchagua vipaumbele kujenga vituo vya afya vya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, je, ni lini vituo hivi vya afya vya kimkakati vitaanza kujengwa, ikiwa ni pamoja na kituo cha afya cha kimkakati kwenye Kata ya Ivuna, ndani ya Jimbo la Momba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Condester Sichalwe kwa kurejea Bungeni na sote tunapaswa kumpa pongezi kwa kutuongezea kijana ndani ya Tanzania yetu, hongera sana. Hongera sana Mheshimiwa Sichalwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati kwenye kata aliyoisema nitahakikisha kwamba, wakati wowote ule tutakapopata fedha tutapeleka kwenye Jimbo la Momba, ili kituo kile kiweze kujengwa na kuhudumia wananchi wa kata ile na pia, wananchi wa Jimbo la Momba. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Itwangi, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Didia**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Didia, ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wa eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, Kata ya Didia ina jumla ya wakazi 19,093. Kata hii inakidhi kigezo cha kuwa na kituo cha afya. Kwa sasa wakazi wa Kata ya Didia wanapata huduma za dharura na upasuaji katika Kituo cha Afya cha Kanisa cha Bugisi. Tunafahamu kwamba, kituo hiki ni cha taasisi binafsi kwa hiyo, wananchi wakienda pale inabidi walipe, hili tunalitambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata za kimkakati zitakazokidhi vigezo, ikiwemo Kata ya Didia katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Azza, swali la nyongeza.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninaomba kurekebisha kidogo, ni Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, siyo Halmashauri ya Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira kuu ya Serikali ya kugawa jimbo na kupata Jimbo jipya la Itwangi ni pamoja na kuhakikisha inasogeza huduma kwa wananchi wake. Kata ya Didia ni miongoni mwa kata kumi zilizomo Tarafa ya Itwangi, ambapo kuna kituo cha afya kimoja tu. Je, Serikali ipo tayari sasa kutuletea fedha kuanza ujenzi kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi mara baada ya Bunge hili, aje Jimbo la Itwangi na Kata ya Didia, ili ajionee shida kubwa tuliyonayo ya kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Jimbo jipya la Itwangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunafahamu kwamba, jimbo hili lenye kata kumi lina kituo kimoja tu cha afya. Kwenye orodha ile ya vituo 94 ambavyo tunatakiwa kupeleka fedha pindi tutakapopokea kutoka Hazina, Kata ya Didia ni moja ya kata hizo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Azza Hillal Hamad kwamba pindi fedha hizi zitakapotoka mara moja tutahakikisha kwamba tunapeleka fedha kwenye Kata hii ya Didia ili kituo kile ambacho kinategemewa na wananchi wengi kiweze kuanza kujengwa na kutoa huduma kwa wananchi wa Kata ya Didia na wananchi wa Jimbo la Itwangi kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari baada ya Mkutano huu wa Bunge kuongozana na Mheshimiwa Azza ili niweze kwenda kuona adha iliyoko kwenye eneo lile na tuone namna ya kuongea na wananchi na kuwahakikishia kwamba tutapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Kata yetu ya Didia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ulizeni maswali mafupi. Mheshimiwa Katani Katani, swali la nyongeza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008 kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru aliweka jiwe la msingi ujenzi wa kituo cha afya Kata ya Mchichira.

Je, lini Serikali itapeleka fedha ikizingatiwa wananchi wale tayari wameanza kujenga wenyewe kituo kile cha afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Kaka yangu Katani kwa namna anavyofanya kazi vizuri. Ni mara nyingi tumekuwa tukijadili mambo kadha wa kadha ambayo tumeyatafutia suluhisho na yeye ni shahidi kwamba kwenye Jimbo lake tumepeleka suluhisho mara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kituo hiki cha afya anachokisema Mheshimiwa Katani, kwa kuwa kimeanza kwa nguvu za wananchi tutapeleka timu yetu kutoka TAMISEMI ili iende ikaangalie pale ambapo wananchi wameshaweka nguvu zao imefika asilimia ngapi ili na sisi kama Serikali Kuu tuweze kutafuta fedha na kwenda kuwasaidia wananchi wa Kata ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Waziri, miaka mitatu iliyopita tulileta majina ya vituo vya mkakati, Kata ya Matui wananchi zaidi ya 30,000 na Kata ya Dongo zaidi ya 28,000. Ni lini tutapata pesa kwa ajili ya kujenga vituo vya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Kaka yangu, Mheshimiwa Olelekaita kwa namna anavyowasemea wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba baada ya kikao hiki leo nikae na Kaka yangu, Mheshimiwa Mbunge, tuweze kuona wapi tumefikia na kama vituo vile vipo kwenye orodha ya vile vituo 94 na kama havipo kwenye orodha tuone namna ambavyo tutalishughulikia jambo hili ili wananchi waweze kupata huduma. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma, swali la nyongeza. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ng'ambo iliyopo katika Jimbo la Tabora Mjini ina wakazi 17,826, haina kituo cha afya wala zahanati. Wakazi hawa wanakimbilia Hospitali ya Mkoa ya Kitete kwenda kupata huduma za afya na eneo tunalo. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanatupelekea fedha ili wananchi wangu waweze kupata huduma za afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza sana Dada yangu Mheshimiwa Hawa, kwa namna anavyofanya kazi, yeye ni shahidi kwamba mimi nilifika jimboni kwake na tulifanya kazi kubwa kwenye Hospitali ya Kitete lakini vilevile kwenye kituo kimojawapo cha afya ambacho kinaendelea kumaliziwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitahakikisha kwamba tunawapeleka timu tukaangalie eneo lile na kuona namna tutakavyolitafutia fedha kama halipo kwenye vituo hivi 94 basi tuone ni namna gani tunavyoweza kuongea na wafadhili tuweze kupata fedha nyingine kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Kukamilisha kazi ya kupeleka Umeme katika Vijiji vya Kwimba**

**MHE. KABULA E. SHITOBELO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Wilaya ya Kwimba, hususan vijiji vya Ng'wambogwa na Kawekamo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kwimba ina jumla ya vijiji 119 ambapo vijiji vyote vimefikiwa na miundombinu ya umeme kuanzia mwezi Disemba 2024. Aidha, jumla ya vitongoji 359 kati ya vitongoji 871 ambavyo ni sawa na 41.22% ya vitongoji vyote vya Wilaya ya Kwimba vimepatiwa umeme na taratibu za kupeleka umeme kwenye vitongoji vilivyosalia zinaendelea na vyote vitakuwa vimepata umeme ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabula, swali la nyongeza.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nyumba zilizofikiwa na umeme kwa vijiji vya Kwimba ni chache sana.

Je, lini sasa Serikali itakamilisha kuweka umeme kwenye kaya zilizobaki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Kabula kwa swali lake zuri na kwa kuwazungumzia wananchi wa Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli lengo la kwanza la Serikali ilikuwa ni kuhakikisha kila kijiji na kila kitongoji kinafikiwa na

umeme, kwa sasa Wizara inao mkakati wa kuhakikisha usambazaji wa umeme katika maeneo ambayo umefika lakini wananchi hawajaingiziwa katika nyumba zao. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, katika bajeti hii ya 2026/2027 tumetenga fedha za kutosha ili kuhakikisha tunasambaza umeme hasa katika vijiji na vitongoji ambavyo umeme umefika ila wananchi wengi bado hawajanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua je, ni lini Serikali itakamilisha kazi ya kupeleka umeme kwenye maeneo ambayo nguzo za umeme zilichimbwa tangu mwezi Agosti, 2025 lakini hakuna kinachoendelea kama vile eneo la Kidiama, Kumulama, Kumuhama, Mrufiti Mpya pamoja na maeneo yote?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupata majibu ya Serikali kwa sababu wananchi wanatamani sana kupata umeme na hasa wakizingatia Serikali imefanya kazi kubwa, imekamilisha Bwawa la Mwalimu Nyerere na uzinduzi umefanyika lakini wao bado umeme haujawafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini kwa kufuatilia kuhakikisha wananchi wake wanapata nishati. Kumbukumbu zangu nilipofanya ziara katika Mkoa wa Kigoma upande wa Kasulu Mjini kulikuwa na changamoto ya mkandarasi ambaye tayari alikuwa ameshalipwa *advance payment* lakini alikuwa anasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatua za kisheria zimeshachukuliwa na mwezi Septemba mwaka huu tutaleta mkandarasi mwingine ili aweze kuendelea na kazi ya kupeleka umeme na atalipwa. Yule alikuwa amelipwa *advance payment* lakini anasuasua huyu mwingine atakayeletwa atalipwa fedha na ninakuhakikishia kabla ya mwaka 2030 vitongoji vyako vyote vitakuwa vimepata umeme. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mimi pia ninapongeza kwa kweli uzinduzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Je, katika Wilaya yetu ya Kilolo tunavyo vitongoji 54 havina kabisa nguzo. Kwa hiyo, wananchi wanasubiri kwa hamu kuona kwamba lini vitongoji hivi vitafikiwa ikiwa ni pamoja na umeme jazilishi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia nimpongeze Mbunge wa Jimbo la Kilolo, mwanamama shupavu anayepambana kwa ajili ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameingia Bungeni tulimpatia vitongoji kadhaa kwa ajili ya kuhakikisha wanapelekewa umeme, lakini Mheshimiwa Waziri ametuelekeza tuongeze vitongoji vingine 20 katika Jimbo lako. Hiyo ni kutekeleza nia ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha vitongoji vyote vinapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuondoa wasiwasi, tutaendelea kutafuta fedha ndani ya Wizara na tutahakikisha kwamba vitongoji vilivyobaki vinakamilika kwa wakati. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbwilo Kapunda, swali la nyongeza.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wakati nchi yetu inasifika kwamba umeme sasa umefika karibu vijiji vyote nchini lakini Kijiji cha Uhuru kilichopo Kata ya Mkinga, Wilaya ya Nkasi hadi leo hii bado hakina umeme na ukizingatia kwamba kijiji hicho kipo kisiwani kina mahitaji maalum.

Je, ni lini sasa Serikali italeta umeme katika kijiji hicho cha Uhuru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza pia Kaka yangu Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa karibu kuhakikisha tunawaangazia wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vitongoji na vijiji ambavyo vipo maeneo ya visiwani, Serikali imezingatia kwa kupeleka umeme, ambapo kwingine tumepeleka umeme wa nishati ya jua, kwingine tumepeleka umeme kwa kupeleka nyaya. Kwa hiyo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, lengo la Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kila mtu anapata umeme na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kijiji hiki cha Uhuru ambacho kipo katika Kata ya Nkasi ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge mikakati inaendelea kuhakikisha tunafikisha nyaya za umeme ili na wao waweze kupata umeme wa Gridi ya Taifa, na Mheshimiwa Mbunge tutakwenda pamoja kuangalia uwezekano wa kuongeza kasi na kuwanufaisha wananchi wa Kijiji cha Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 6

**Kupeleka Umeme kwenye Vitongoji Visivyo na Umeme – Tunduru**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye vitongoji visivyo na umeme Wilayani Tunduru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tunduru ina jumla ya vitongoji 1,178, ambavyo hadi kufikia mwezi Agosti, 2026 vitongoji 841 sawa na 71.39% vimefikiwa na huduma ya umeme. Aidha, wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji Awamu ya Pili 'A' na 'B' katika vitongoji 236 vya Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali kupitia *REA* inaendelea na maandalizi ya mradi wa *Universal Hamlet Electrification and Last Mile Connectivity Project* ambapo tunalenga kupeleka umeme katika vitongoji vyote vilivyosalia nchini ifikapo mwaka 2030. Mradi huu utatekelezwa kwa njia ya *framework contract* ambapo kwa awamu ya kwanza vitongoji 40 vimepangiwa kupatiwa umeme katika Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, swali la nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi na kwa majibu mazuri ambayo yametolewa na Naibu Waziri lakini ninayo maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba tufanye masasahihisho. Kwenye vitongoji Wilaya ya Tunduru viko vitongoji 1,179 na siyo 1,178 lakini vitongoji ambavyo havijafikiwa umeme siyo 236, vitongoji ambavyo havijafikiwa umeme ni 331.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo umeyasema Mheshimiwa Naibu Waziri, ninatamani kujua ni nini sasa mkakati wa Serikali wa dharura wa kuhakikisha vitongoji hivi navyo vinapatiwa wa umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, pale katika Halmashauri ya Tunduru kuna mradi mkubwa wa umeme ambao unatekelezwa, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alikuja hivi karibuni, aliona jinsi ule mradi unavyosuasua katika utekelezaji. Mradi ule kama utakamilika sisi Tunduru tunanufaika, Mkoa wa Mtwara kwa maana ya Masasi na Nanyumbu watanufaika. Ninatamani kujua ni nini sasa mkakati wa Serikali kwa kuwa hata yule mkandarasi ameonekana anafanya kazi kwa kusuasua.

Je, ni lini tutapeleka pesa ili kuhakikisha ule mradi unakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana na mimi tangu mwaka huu uanze mkakati wa kuhakikisha vitongoji vyote vinafikiwa na umeme umekuwa kama mkakati wa dharura. Kwa mara ya kwanza tangu Wizara ya Nishati iumbwe mwaka huu ndiyo tumesaini mkataba mkubwa wa kupeleka vitongoji zaidi ya 9,000 wenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.2. Huo ni mkakati mkubwa wa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tayari mkataba ulisainiwa na vitongoji vingi tunapeleka, baada ya kupitisha bajeti hii tumeongeza vitongoji vingine 20 kwenye kila Jimbo. Hilo Mheshimiwa Mbunge utakubaliana na mimi kwamba hii ni mikakati ya dharura ambayo Wizara ya Nishati kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu tunafanya kuhakikisha

kwamba tunafika mwaka 2030 tukiwa tumekamilisha vitongoji vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge pia atakubaliana na mimi kwenye swali lake la pili kuhusiana na mradi wa kujenga *transmission lane* Tunduru – Masasi kwa ajili ya kuwaingiza mikoa ya Lindi na Mtwara katika gridi ya Taifa. Kweli mradi ule ulikuwa unasuasua kwa sababu tulikuwa hatujapata fedha, lakini sasa mkandarasi amelipwa na Mheshimiwa Waziri ameshakwenda zaidi ya mara tatu katika eneo lile na mlikwenda naye Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kazi hii inakwenda kwa kasi, kwa sababu lengo tunataka kabla mwaka huu haujaisha Mikoa ya Lindi na Mtwara iweze kuingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia kuwa nia ya dhati ipo na Mheshimiwa Waziri anatukimbiza kila siku na tunavyo vikao vya mara kwa mara kuhakikisha kwamba mkandarasi yule hasimami na maeneo ya Lindi na Mtwara yanaingizwa katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Mahera, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaanza kuipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri mnayofanya kusambaza umeme vijijini. Wilaya ya Butiama ina vitongoji 109 ambavyo havina umeme hasa kwenye Kata muhimu sana kama vile ya Buhemba, Buruma, Muriaza, Bukabwa, Masaba, Kyanyari na Bwiregi.

Je, lini Serikali itakamilisha upelekaji wa umeme katika vitongoji hivyo katika Kata hizo muhimu katika Jimbo la Butiama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali nzuri na ninakupongeza kwa kufuatilia kwa karibu kwa sababu Jimbo lako ni miongoni mwa Majimbo ambayo yamebakiza vitongoji vichache sana ambavyo havijafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Wizara ya Nishati tutahakikisha vitongoji vilivyobaki vinakamilika kabla ya mwaka 2030. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais iko katika Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, iko katika Dira 2050. Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi, tutajitahidi kukamilisha kwa wakati ili na wewe uweze kukaa kwa amani katika Jimbo lako. Nakushukuru.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ninaipongeza Serikali pamoja na Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rorya kati ya vitongoji 508 vitongoji ambavyo vina umeme ni 189 peke yake, zaidi ya 60% ya vitongoji katika 508 havina umeme. Hivi karibuni kwa kuwa mmefanya utafiti kwamba mkandarasi anaingia *site* kwa ajili ya kupeleka umeme vitongoji 74 na mpaka sasa hajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nijue lini mkandarasi huyu atafika *site* kwa ajili ya utekelezaji wa umeme kwa vitongoji hivi 74 katika Wilaya ya Rorya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rorya. Baada ya kusaini mkataba sasa hivi tuko kwenye hatua ya manunuzi ya vifaa na ninakuhakikishia wakandarasi wataanza kuingia *site* ndani ya mwezi huu na mwezi ujao, vitongoji vingi siyo tu cha Mheshimiwa Chege, vitongoji vingi vitaanza kuvutiwa umeme na vile ambavyo bado tunaendelea kufanya *survey* ili viweze kutafutiwa bajeti na kupelekewa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Baraka Mwamengo, swali la nyongeza.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuniona. Ninaomba niulize swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo la Kyela kuna vitongoji ambavyo vina watu wengi na havijapata umeme mpaka leo. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji hivyo ikiwemo vya Kata ya Ngonga, Ngana na baadhi ya maeneo ya Lusungo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Baraka, Mbunge wa Kyela kwa kufuatilia kwa karibu kuhakikisha suala la kupeleka umeme kwenye vitongoji vyake 52 vilivyobaki unakamilika kwa wakati. Mheshimiwa Baraka ni kwa sababu ya umakini wako na wewe ni mmoja kati ya Majimbo ambayo kwa kweli vitongoji ambavyo vimebaki ni vichache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na vitongoji ambavyo tayari tumeshakupatia mwezi Februari mwaka huu, tumekuongezea vitongoji vingine 20 ambavyo sisi pamoja na wewe tuliketi na kukubaliana na vile ambavyo vimebaki tutaendelea kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba vinapatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji.

Ninamwita Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 7

**Wananchi wa Korogwe kupata Maji ya Mradi wa Same – Mwanga – Korogwe**

**MHE. CHARLES M. NJAMA** aliuliza:-

Je, lini wananchi wa Korogwe Mjini wataanza kupata maji kutoka kwenye Mradi wa Same – Mwanga – Korogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Injinia Mathew Andrea Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji, Same – Mwanga – Korogwe kwa kutumia chanzo cha Bwawa la Nyumba ya Mungu lililopo Wilaya ya Mwanga Mkoani Kilimanjaro kwa gharama ya shilingi bilioni 406. Mradi huo kwa sasa unanufaisha zaidi ya wananchi 96,213 waishio katika Miji ya Mwanga na Same sambamba na vijiji 10 vya Wilaya hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2026/2027, Serikali itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kufikisha huduma ya maji kwenye maeneo yote yaliyobaki ikiwemo vijiji vitano vya Wilaya ya Korogwe, baada ya usanifu kukamilika, Serikali itaanza kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa awamu zote mbili za mradi wa Same – Mwanga – Korogwe kunalenga kuhudumia zaidi ya wananchi 456,931 waishio katika Miji ya Same na Mwanga sambamba na vijiji 38 ambapo kati ya hivyo, vijiji 21 ni vya Wilaya ya Mwanga, vijiji 12 ni vya Wilaya ya Same na vijiji vitano vikiwa katika Wilaya ya Korogwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mhando Njama, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, ninamshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Korogwe Mjini lina miradi mikubwa miwili ya maji. Tunao mradi wa Ndemaha ambao umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni mradi wa kulaza mabomba kutoka kwenye chanzo cha maji mpaka kwenye chujio, lakini pia na chujio. Mradi huu umesimama kwa muda mrefu kwa sababu ya kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi ambaye anadai shilingi 222,000,000 na mabomba yamefika karibia miezi mitatu mpaka sasa, bado hayajaanza kulazwa.

Je, ni ipi kauli ya Serikali kuruhusu kufanya malipo na kuruhusu mradi huu uendelee?

Swali la pili; tunao mradi mkubwa wa Miji 28 ambao ni tegemeo kubwa kwa ajili ya kuondoa kero ya maji tuliyokuwa nayo kwa muda mrefu katika Mji wetu wa Korogwe Mjini. Mradi huu umekuwa na ahadi nyingi za kumalizika, tulitazamia kupata maji mwezi wa tatu, baadaye tukaambiwa mwezi wa saba, na sasa tumeambiwa ni mwezi wa kumi lakini bado kuna *risk* ambayo inaonekana, kwa sababu mkandarasi mdogo aliyepewa kazi ya kulaza mabomba, ameshindwa kufanya kazi hiyo kwenye Mto Pangani katika eneo la Tingetinge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge uliza swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Je, ni lini watu wa Korogwe Mjini watazamie sasa kupata maji kutoka katika mradi huu wa miji 28 ambao ni tegemeo kubwa kwa kuondoa kero hiyo ya maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Charles Mhando Njama kwa

kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika Jimbo la Korogwe Mjini, hakika mafanikio yameanza kuonekana kwa kuanza kutekelezwa kwa miradi hii miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa kwanza wa ujenzi wa chujio katika Mji wa Korogwe ambapo ni juhudi za Mheshimiwa Mbunge ambao una zaidi ya shilingi bilioni 1.048, ni matokeo ya kazi kubwa ya maombi ambayo aliyafikisha kwa Mheshimiwa Rais na hatimaye mradi huu kuanza kutekelezwa na sasa uko katika *status* ya 15%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu pia kuna hii sehemu ambayo amesema ya Ndemaha, mradi huu wa Ndemaha wa kutoa maji kutoka kwenye chanzo kwenda kwenye eneo la chujio wenye gharama ya shilingi bilioni 1.81, ni kweli kabisa kwamba miradi hii haiendi kwa *speed* inayotakiwa. Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba, mkandarasi huyu kwanza haidai Serikali lakini changamoto ni kwamba hana uwezo wa kujitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Maji, kumweleza Katibu Mkuu kufanya *assessment* kuhusu huyu Mkandarasi kwa sababu hatakiwi kuchelewesha kazi ya wananchi wa Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba tunakaa karibu, tutakuwa tunafanya *monitoring and evaluation* ili kujiridhisha na mwenendo wa Mkandarasi. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawalinda wakandarasi wa ndani lakini na wao watoe matokeo ambayo tunayatarajia katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa Miji 28, Mradi huu wa Korogwe – Handeni – Muheza pamoja na Pangani wenye gharama ya shilingi bilioni 171 sasa umefikia 84%. Tunatambua ipo changamoto *sub-contractor* aliyekuwa amepewa kazi, ikaonekana kwamba hana uwezo wa kujitosheleza wa kutatua changamoto ya kulaza mabomba katika Mto wa Pangani pale, tumemwelekeza Mkandarasi ahakikishe kwamba anapata *sub-contractor* mwenye uwezo na kwa haraka sana ili kuhakikisha kwamba mradi huu unaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Mheshimiwa Mbunge kila siku ni kuhakikisha kwamba maji yanatoka na wananchi wa Korogwe wanapata maji, sisi tunahakikisha kwamba tunaenda kutekeleza ili maji yaweze kutoka kwa wakati na wananchi wa Korogwe Mjini waweze kunufaika na huduma hiyo ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipatia fursa nami kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mji wa Tarime ambao wana mitaa 81, zaidi ya 50% hawapati maji safi na salama hawana maji kabisa ya kuunganishwa kwa bomba. Na kwa kuwa, tunao mradi wa Ziwa Victoria ambao ulitarajiwa kukamilika Septemba lakini hamna uwezekano wa kukamilika Septemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni sasa irudishe ile huduma ya *RUWASA* kama vile watu wa Nishati wanavyofanya kwenye mitaa yenye sura za vijiji wanatuletea umeme wa *REA* na kutuunganishia kwa bei ya shilingi 27,000? Mturudishie huduma ya *RUWASA* ili hii ya zaidi ya watu 51% waweze kuchimbiwa visima wakati wakisubiri huu mradi wa Ziwa Victoia ambao hauwezi kukamilika mwaka huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na ni maombi ya Mheshimiwa Mbunge, na tunatambua kwamba upatikanaji wa maji katika Mji wa Tarime Mjini, unategemea sana ukamilikaji wa mradi wa shilingi bilioni 134 ambao unatekelezwa kutoka Rorya, Tarime pamoja na kwa Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi na imekuwa ndoto ya Mheshimiwa Esther Matiko, kuwa na mamlaka ili waweze kujiendesha katika Mji wa Tarime. Sasa kuwarejesha *RUWASA* waanze kuhudumia pale ile ndoto yake pia inaweza ikafa palepale. Kwa hiyo, tunachohitaji sasa ni kupeleka fedha na kwenda kuimarisha mifumo ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Tarime Mjini wanaanza kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu kwamba tunao mkakati ambao tumejipanga kwenda kuhakikisha kwamba tunatumia mikakati ya dharura ili wananchi wa Tarime Mjini waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Tarime hawahitaji kujua nani anawapatia maji, isipokuwa wanahitaji maji ili waweze kunywa yakiwa safi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Biharamulo kuna miradi mikubwa ya maji inayoendelea katika Kata ya Nyakahura, Kata ya Rusahunge eneo la Nyakanazi na Kata ya Nyarubungo, ni miradi mikubwa, mingi zaidi ya shilingi bilioni moja. Mradi mmoja wa Nyarubungo ni 1.4, Nyakahura ni 1.4, lakini ule wa Nyakanazi ni 2.9 bilioni, kwa hiyo ni miradi mikubwa ya kimkakati kwa eneo la kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejikuta kwamba ile miradi yote imekwama kwa sababu mtekelezaji wa ile miradi ni mmoja na amejitahidi sana kufanya kazi, lakini ana madai ya muda mrefu Wizarani hali ambayo imemsababisha amekuwa *incapacitated* kiasi kwamba hawezi tena kuendelea na ile miradi, na miradi imefikia katikati haiwezi kutoa maji kwa sababu ana madai yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninataka nisikie kauli ya Serikali, ni lini mtu huyo atalipwa ili nia njema ya Serikali ya

kuwapelekea wananchi wa Biharamulo maji iweze kutimilika kwa vile anakwama kwa sababu ya malipo?

**NAIBU SPIKA:** Karibu Waziri kwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana, kazi kubwa anayoifanya na hata hii miradi asingekuwa anaifuatilia kwa ukaribu isingeweza kuanza na sasa imeanza. Hiyo ni hatua moja kubwa ambayo ninampongeza sana na sisi Wizara ya Maji tutahakikisha kwamba tunampa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupitisha sheria ambayo imetufanya tuweze kupata fedha za tozo ya mafuta moja kwa moja zaidi ya 70%, ambayo sasa itatufanya tuweze kupangilia mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikujulishe kwamba kuanzia mwezi huu tayari tumeanza kupokea fedha na tayari tumeanza ku-*disburse* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunalipa madeni katika miradi yote inayoendelea nchini. Tunafahamu kwamba *burden* ni kubwa, fedha inayokuja haiwezi kutosha kwa pamoja, nimtoe hofu kwamba tunaenda kumuweka kwenye vipaumbele kuhakikisha kwamba miradi yake na mkandarasi wake analipwa kwa wakati ili aende kutekeleza mradi huo na ukamilike kama ambavyo amekusudia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**MHE. MARIAM A. MUNGULA K.n.y. MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Ninaomba sasa swali Namba 8 la Mheshimiwa Asha Baraka, lipewe majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam, ngoja nikuite kwanza. Swali la Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mariam Mungula, karibu.

Na. 8

**Kumaliza Migogoro ya Ardhi Nchini**

**MHE. MARIAM A. MUNGULA K.n.y. MHE. ASHA R. BARAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaunda Tume itakayotatua migogoro ya ardhi nchi nzima?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali Na. Nane la Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa migogoro ya ardhi, kufuatia hali hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, aliekeleza Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuandaa mapendekezo yatakayowezesha kupata suluhisho la kudumu la migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizobainishwa, imeandaa rasimu ya mkakati wa utambuzi wa

migogoro ya ardhi nchini, utekelezaji wa mkakati huo utahusisha wadau wote muhimu katika utatuzi na udhibiti wa migogoro ya ardhi. Aidha, mkakati huo utakuwa na kanzidata moja ya migogoro ya ardhi, hivyo kuimarisha uelewa, uwazi, uwajibikaji na kasi katika kushughulikia migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile utekelezaji wa mkakati utaimarisha amani, umoja na mshikamano katika jamii hivyo kuboresha mazingira ya uwekezaji katika ardhi na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Mungula, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM A. MUNGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru tena kwa kunipa nafasi hii, nina maswali mawili madogo ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Swali Namba Moja, kwa kuwa suala la umiliki wa ardhi linasababisha migogoro mingi kutokana na *double allocation*, Serikali inachukua hatua gani kukomesha tatizo hili la hatimiliki za ardhi kutolewa mara mbili au zaidi kwa watu tofauti?

Swali Namba Mbili, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha mfumo wa usajili wa ardhi ili kuzuia migogoro ya aina hii kuendelea kujitokeza? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali kwa sababu nimeona dhamira ya dhati ya kuungana na Wizara katika kumaliza au kupunguza migogoro ya ardhi inayoendelea hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya *double allocation* ipo na imeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu mwanzoni kulikuwa na mifumo ambayo ilikuwa na changamoto

ambayo kulikuwa na uwezekano wa kuomba na kupata huduma hiyo. Kutokana na mwingiliano mkubwa wa mahitaji ya ardhi katika baadhi ya Miji hususani hapa Dodoma, kulikuwa na mkanganyiko wa watu kuuza ardhi kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, tunalishukuru sana Bunge lako pia tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu amewezesha uwepo au kujengwa kwa mfumo wa *e-Ardhi* ambao hakutakuwa na changamoto tena ya *double allocation*, zile changamoto zote ambazo zilitokeza katika mifumo ya awali, tayari imeshazuiwa huwezi tena kupata changamoto ya *double allocation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa mmiliki yeyote wa ardhi, sasa ni wakati husika wa kuomba umiliki halali na kuweza kupata hati, hii itasaidia pia yeyote ambaye anakuwa na ardhi bila kuiendeleza, ndiyo mwingiliano huu wa utapeli wa kuweza kuuza kwa watu wawili, watatu unaweza kutokea.

Swali Namba Mbili kuhusu mfumo wa upatikanaji wa hati na usajili, sasa hivi tayari tumeshamaliza kuandaa na kutengeneza mfumo huu, hatua inayofuata ni kuusambaza katika Mikoa mbalimbali. Mpaka sasa hivi, Mikoa mitano tayari tumeshaisambaza lakini ndani ya mwaka huu wa fedha, kwa kutumia Bunge hili, tulipata fedha ambayo tutaweza kusambaza mifumo hii kwa Mikoa mingine aliyobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edibily Kinyoma, swali la nyongeza.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu ahadi yake ya kurudi Kasulu Vijijini na timu yake na watu wa Maliasilili kumaliza migogoro ya Kasulu Vijijini kabla ya msimu wa kilimo kuanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Kusini, kimsingi ameshirikiana sana na mimi katika kunikumbusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, safari hii ilihusisha Waheshimiwa Mawaziri zaidi ya mmoja, kwa hiyo, ilikuwa ni changamoto ya kupata ratiba moja. Mimi ninaendelea kukuahidi, bado maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wangu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yako palepale, kuwa tutakuja Kigoma. Pia tunaendelea kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, kuendelea kutuliza hali ambayo ipo, wananchi waendelee kuwa na utulivu na kufanya kazi zao za kiuchumi. Hivyo nikuhakikishie, tutaendelea kuwasiliana na wewe na Waheshimiwa Mawaziri wengine, tutakuja kwenye maeneo na tutaendelea kutatua changamoto kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Chakoma, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya ardhi nchini imekuwa ni tatizo kubwa kiasi cha kusababisha baadhi ya familia kupoteza ardhi na kuingia kwenye dimbwi la umaskini.

Ni ipi kauli ya Serikali juu ya mgogoro unaoendelea kati ya mwekezaji *Transcontinental Ford Limited* na wananchi wa kijiji cha Lupunga Kata ya Kikongo Wilayani Kibaha, Mkoani Pwani? Ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi ina vyanzo vingi ambavyo kimoja wapo ni mwingiliano wa matumizi ya ardhi, kugombania mipaka, pia kutozingatia mpango wa matumizi ya ardhi. Kwa swali la Mheshimiwa Mbunge alilouliza, mimi ninaendelea kumshukuru kwa sababu amelikumbusha katika Bunge hili. Migogoro kama hiyo tayari imeshapatiwa nguvu kazi ya kwenda kufanyiwa utambuzi na kusikiliza wananchi walio katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimwakikishie tu baada ya kupata nafasi na Mheshimiwa Waziri kutoa ridhaa, tutaenda kwenye maeneo yake na kwenda kutoa tamko la Serikali ili mgogoro huo uishe. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 9

**Uhai na Uwepo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. MARYAM USSI YAHYA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha uhai na uwepo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikizingatiwa kuwa malipo ya michango ya nchi wanachama yamekuwa yakisuasua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa James Millya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. JAMES K. MILLYA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu

tangu niteuliwe kuwa Naibu Waziri, ninaomba kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Chama chetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Heshima hii ni kubwa na isionekane ni aibu kusema tangu dunia iumbwe, na tangu uhuru wa nchi yetu utokee, ni mara ya kwanza tangu Jimbo hili lipate uteuzi wa namna hii, tunachukua kwa heshima na unyenyekevu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia, kwa namna ya kipekee, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Simanjiro, ambao wamenirejesha Bungeni, nami ninawashukuru ninasema ahsanteni sana. Ninaomba niseme kwamba heshima hii siyo ya bure, ninaiheshimu na mimi nitoe ahadi yangu kwamba nitaitumikia Serikali hii na Watanzania kwa ujumla na kusema nitatenda kazi zangu kwa uzalendo mkubwa na unyenyekevu wa kipekee, ahsanteni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na Waheshimiwa Wabunge ninawashukuru kwa namna ambavyo mmenipa ushirikiano tangu niteuliwe mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imeendelea kulinda na kutetea maslahi ya Taifa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuhakikisha kuwa, Jumuiya inaendelea kuimarika na kunufaika kupitia utekelezaji wa programu za maendeleo, ukuaji wa biashara, ongezeko la uwekezaji katika miundombinu na huduma za kijamii kama vile afya, elimu, sekta za uchumi za viwanda, nishati, kilimo, mifugo, uvuvi, miundombinu, maji, utalii, upatikanaji wa ajira na kuchangia kuimarika kwa ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na manufaa yanayopatikana, changamoto kubwa inayoikabili Jumuiya kwa sasa ni michango ya baadhi ya Nchi Wanachama kutotolewa

kwa wakati na ukamilifu hali inayoathiri utekelezaji wa shughuli na programu za Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua katika kuhakikisha kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea kuwa hai na inatekeleza kikamilifu majukumu yake. Mathalan, Tanzania ilikuwa sehemu ya maamuzi ya Mkutano wa 25 wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* uliofanyika Machi, 2026 ambao uliidhinisha mfumo mpya wa uchangiaji ambapo 50% ya mchango utatolewa kwa usawa na kila Nchi Mwanachama na 50% utatokana na uwezo wa nchi wa kiuchumi *(GDP)*. Mfumo huu umeanza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania kama mwanachama hai na mwaminifu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tayari imeshatoa mchango wake wa mwaka huu wa fedha 2026/2027 kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM USSI YAHYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninamshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Millya kwa majibu yake mahiri. Nina swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwamba Tanzania imeshalipa kwa asilimia mia moja, lakini je, ana taarifa yoyote kwamba Wabunge wa Afrika Mashariki hawajalipwa ndani ya miezi sita, na kama anayo, je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Wabunge hawa wanapata stahiki zao kwa muda mwafaka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. JAMES K. MILLYA):** Mheshimiwa Naibu

Spika, kwanza kabisa ninaomba kipekee nimpongeze Mheshimiwa Mariam Ussi kwa namna ambavyo mara nyingi anafuatilia masuala yake na masuala haya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mambo ya Nje kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba swali hili ni zuri, lakini kwa kuwa mwanadiplomasia namba moja, pale Arusha Machi, 2026 mwaka huu katika Mkutano wa 25 wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania kwa diplomasia ya kipekee iliyojengwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari imepata Katibu Mkuu kwa mara nyingine ya pili wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Balozi Stephen Mbundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara, tunalichukua hili kama changamoto ya wanachama 6,000 ambao waliwahi kutumika kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunaenda kufuatilia kwa umahiri. Kwa kuwa usukani huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki upo mikononi mwa Tanzania, mnamfahamu Mheshimiwa Rais ni mtu mnyenyekevu; mnaifahamu Jumuiya ya Afrika Mashariki, Marais wote ambao wanaunda Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni watu mahiri wanaojali masilahi ya wanachama wote na nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Naibu Waziri ninayehusika na sehemu hii ya Mambo ya Nje, nipo tayari kufuatilia na nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba iwapo atahitaji mimi na yeye kukaa ili kubainisha, kwa sababu pia miongoni mwa watu waaminifu huwezi kukosa wawili watatu ambao wanaweza wakapotosha, lakini nipo tayari kukutana naye na kuweza kubaini kwa umakini na kwa uangalifu ili niweze kufuatilia kwa hatua stahiki. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Imamu Vuai, swali la nyongeza.

**MHE. IMAMU MTUMWA VUAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Je, Serikali haioni haja ya kuishauri Jumuiya kuanzisha mfumo wa vyanzo vya mapato vya kudumu badala ya

kutegemea michango ya wanachama ambayo inachelewa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. JAMES K. MILLYA):** Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe kuwaambia Watanzania kwa ujumla kwamba Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Machi, mwaka huu 2026, mambo mengi yanapitiwa, na sisi kama Baraza la Mawaziri ambalo linahusika na Jumuiya, tunaangalia namna kubwa ya kuiokoa Jumuiya yetu. Itoshe pia kuwafahamisha kwamba mbali na biashara ambayo inaweza ikafanyika, lakini Watanzania wafahamu mahali peke yake ambapo Tanzania inapata urari *positive* wa biashara ni kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024, Tanzania iliuza bidhaa karibu dola za Kimarekani bilioni 1.2, lakini leo hii 2025 takwimu zinaonyesha kwamba tumeuza takribani bidhaa za shilingi bilioni 1.26, maana yake Jumuiya hii ni muhimu kwa biashara za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri pia kuwaambia Watanzania kwamba kwenye Jumuiya hii ya Afrika Mashariki ndipo ambapo mkulima wa kawaida, muuzaji wa mbogamboga, maharage, na nyama wanapouza. Kwa hiyo, ni sehemu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo tayari kama Serikali, na kama Jumuiya kwa ujumla kukaa chini na wadau wote. Mheshimiwa Mbunge niko tayari kukaa na wewe. Mawazo ambayo yanajenga Jumuiya yetu, tuko tayari kuyatumia ili tuweze kuimarisha Jumuiya yetu. Ukweli ni kwamba kwenye uanzishwaji wa Jumuiya, tunatambua kwamba kuna makosa yalifanyika kwenye kugawa Bara la Afrika; tunahitajiana, Maasai wa Longido na Maasai wa Namanga ni wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kule upande wa Kenya kuelekea upande wa *South Sudan,* makabila ni yale yale. Kwa hiyo, Jumuiya siyo ya kibiashara peke yake, bali ni kuweka

undugu ambao Wakoloni wetu walitutenganisha. Kwa hiyo, tunahitajiana kuliko kitu chochote. Mimi nipo tayari, kwa mawazo yoyote ya kujenga, Serikali ipo tayari kusikiliza mdau yeyote na tupo tayari kufanyia kazi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Madini, ninamwita Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Vibali vya Kuchimba Madini Kwenye Hifadhi**

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaruhusu wananchi kupewa vibali vya kuchimba madini kwenye hifadhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 26 cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323, uchimbaji wa madini ndani ya Hifadhi za Misitu zinazosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* unaruhusiwa pale ambapo mwombaji amepewa leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria hiyo na amekamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assessment - EIA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mapori ya akiba yanayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori

Tanzania *(TAWA)*, Vifungu vya 20(2) na 20(3) vya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283, vinazuia utafutaji au uchimbaji wa madini ndani ya pori la akiba isipokuwa mafuta, gesi asilia na madini ya urani, baada ya kufanyika ya kuwa kumefanyika *EIA* na kulipwa gharama za ulinzi wa eneo, ada ya leseni, na Serikali kuwa ndiye mwanzilishi wa mradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kifungu cha 120(1) (c) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123, kinamtaka mmiliki wa leseni ya madini kupata ridhaa ya maandishi ya mamlaka zinazosimamia Hifadhi za Misitu, pori la akiba, eneo la hifadhi ya malisho au eneo lingine la hifadhi kabla ya kutumia haki zake za madini katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Serikali itaendelea kutoa vibali vya uchimbaji wa madini katika maeneo ya hifadhi yanayoruhusiwa kisheria kwa wananchi na wawekezaji watakaokidhi masharti husika na kupata vibali kutoka *TFS, TAWA* na *NEMC,* kadiri maombi yanavyowasilishwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni lini Serikali itajikita katika utafiti wa kina wa maeneo ya uchimbaji wa madini hususan katika Mkoa wa Morogoro ili tuweze kuchimba kwa utaratibu na kuacha kuchimba kiholela?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Serikali ina mkakati gani wa kuzishughulikia zile leseni ambazo zimetolewa, lakini haziendelezwi kwa wakati ambazo zinachochea uchimbaji haramu na uvamizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Josephine kwa jinsi ambavyo amekuwa mtetezi wa kweli wa wachimbaji wadogo wa madini

nchini. Nitumie fursa hii kumjibu kwa swali lake la kwanza kuhusu mpango wa Serikali wa kuongeza wigo wa utafiti ili kubaini maeneo yenye madini ya aina mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba zoezi hili linaendelea na hivi sasa Serikali iko katika hatua za mwisho za kupata kampuni kubwa ya utafiti wa madini kwa kutumia ndege ya nyuki na ndege nyingine kubaini maeneo yote yenye madini kwa kumulika kutoka juu ile tunayoita *high resolution aerial surveying* ili kujua maeneo sahihi ya kuwapa wachimbaji wetu wadogo, wakubwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, niendelee tu kusisitiza kwamba Watanzania wachangamkie fursa za kutafuta maeneo ya uchimbaji wa madini kwa sababu Serikali inaenda kuwafanyia utafiti na muda siyo mrefu tutakuwa na maeneo sahihi yenye taarifa sahihi za kuwapa wachimbaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili kuhusu leseni ambazo hazijaendelezwa, ninapenda tu kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna kaguzi zinazoendelea. Kuna zoezi linaendelea la kukagua leseni zote nchini ili kubaini maeneo ambayo hayaendelezwi na hati za makosa kutolewa na kufutwa kwa leseni hizo. Hivi sasa tupo katika hatua ya kufuta leseni 87 ambazo zikishafutwa kwa mujibu wa sheria kuna maeneo matano ambayo yatatengwa mahsusi kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nitoe rai kwa wamiliki wa leseni nchini waendeleze leseni zao kwa sababu wasipoendeleza, tutazifuta na wale ambao wako tayari kuwekeza waje wayaombe hayo maeneo baada ya kuwa yamefutwa na kutangazwa na Serikali. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya swali la nyongeza. Kwa kuwa maeneo yanayozunguka Wilaya ya Urambo yana madini yakiwemo dhahabu, ambalo ni jambo zuri na muhimu. Je, ni lini Serikali itafanya utafiti katika Wilaya ya Urambo ili kugundua madini

yaliyopo ili wananchi wa Urambo nao wanufaike na madini waliyonayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, madini.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza mama yangu, Mheshimiwa Sitta kwa swali lake zuri na amekuwa akitufuata mpaka kwenye ofisi zetu akiulizia fursa za uwekezaji kwenye sekta ya madini kwa ajili ya wananchi wake wa Jimbo la Urambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumjulisha mama yangu kwamba hivi sasa katika Wilaya ya Urambo, aina pekee ya madini ambayo yanaendelea kuchimbwa na kuzalishwa ni madini mchanga. Kuna leseni nne ambazo ziko na zinafanya kazi, lakini juhudi za kufanya utafiti ili kubaini madini mengine yanayopatikana katika Wilaya hiyo, ziko katika mpango mahususi wa Serikali wa kanda ambao utaenda kufanyiwa utafiti wa kina wa kutumia ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kwenye jibu la msingi, ni kwamba kuna utafiti utakuja kufanyika ambapo utafiti huo utafanywa katika Mikoa ya Katavi, Tabora, Kigoma, Geita na mpaka katika maeneo ya Rukwa. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba baada ya utafiti ule kukamilika, basi Wachimbaji wa Urambo ambao wapo tayari watapata maeneo ya kwenda kufanya uchimbaji wa madini aina nyingine. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwamba tarehe 31 wataenda Nyamongo na ndege ya nyuki kuangalia maeneo, kutafuta wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hifadhi ya Serengeti, Kata ya Kwihancha, Gorong'a, Nyanungu na vijiji saba inasemekana kuna madini pale na tunapata madhara ya vijana wetu kwenda Kenya, wanapoteza maisha na zaidi ya watu 16 wameshakufa.

Ningeomba nijue ni lini Serikali itafanya utafiti katika maeneo yale halafu vijana wa eneo lile wapate nafasi ya kuchimba na kunufaika ili kunusuru maisha yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waitara kwa sababu amekuwa mtetezi wa kweli wa wachimbaji na msemaji mzuri sana katika sekta yetu ya madini. Ningependa kumjulisha tu kwamba kwa mujibu wa sheria zetu na matumizi ya maeneo mbalimbali yaliyotengwa nchini kama ni ya hifadhi, kama ni malisho, taratibu zinavyozingatiwa kwa eneo ambalo lina manufaa makubwa ya kiuchumi na aina nyingine ya uwekezaji ambao una tija zaidi kwa Taifa, kuna utaratibu wa kuweza kuyatenga maeneo hayo kwa ajili ya wachimbaji ambao wako tayari kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mfano hai, katika madini ya *uranium* ambayo yanachimbwa katika eneo la Mto Mkuju, eneo lile lilikuwa ni sehemu ya Pori la Akiba la Selous ambalo baadaye limekuwa la Hifadhi ya Mwalimu Nyerere na sasa tunakwenda kuchimba madini ya *uranium* kwa sababu taratibu za kisheria zimefuatwa, eneo likatengwa kwa ajili ya uchimbaji katika eneo hilo. Hivyo, katika eneo la Serengeti, taratibu hizo zikiweza kuzingatiwa na tathmini zikafanyika, uwezekano wa kupata maeneo upo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swali lake.

Na. 11

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu na Intaneti Vijijini**

**MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka mitandao ya simu na intaneti Kata za Ruaha, Sali, Vigoi, Kichangani, Iragua, Ilonga, Mbuga na Euga – Ulanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ilizijumuisha Kata za Ruaha, Sali, Vigoi, Iragua, Ilonga, Mbuga na Euga katika miradi ya mawasiliano ya awamu mbalimbali iliyotekelezwa kuanzia mwaka 2016. Katika awamu hizo mawasiliano yalifikishwa katika Kata za Ruaha *(TTCL)*, Sali *(Yas)*, Euga *(Airtel)*, Iragua *(TTCL na Halotel)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kata ya Vigoi inahudumiwa na *Yas* pamoja na *Airtel*. Pamoja na jitihada tajwa, baadhi ya maeneo yaliendelea kuwa na changamoto za kukosa huduma za mawasiliano na hivyo kupelekea Serikali kuifanyia kazi changamoto husika. Kwa sasa, utekelezaji unaendelea katika Kata ya Ruaha *(Airtel)*, Kata ya Euga *(Vodacom)*, Kata ya Ilonga *(Vodacom)* na Kata ya Mbuga *(TTCL)* ambapo utekelezaji utakamilika mwezi Machi, 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada nilizotangulia kuzitaja, Serikali kupitia *UCSAF* itafanya tathmini katika Vijiji vya Kata za Sali, Vigoi, Kichangani na Iragua kwa ajili ya kuangalia mahitaji halisi ya kufikisha huduma za mawasiliano kwa maeneo yatakayobainika kuwa na changamoto ya huduma za mawasiliano. Hivyo, maeneo yote yatakayobainika yataingizwa katika utekelezaji wa kupatiwa huduma za mawasiliano katika mwaka huu wa fedha wa 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, swali la nyongeza.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kwenye maswali nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali haioni umuhimu wa usambazaji wa mitandao ya simu na *internet* katika vijiji vyote vya Tanzania kama walivyofanya kwenye umeme wa *REA?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ninaomba urudie kwa sauti. Mheshimiwa Naibu Waziri hajakusikia vizuri.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni umuhimu wa usambazaji wa mitandao ya simu pamoja na *internet* katika vijiji vyote vya Tanzania kama ambavyo walifanya kwenye umeme wa *REA? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu mkubwa wa kusambaza huduma za mawasiliano kote nchini, lakini tumeandaa mkakati wa Wizara kwa miaka mitano. Tumeshafanya tathmini, na mpaka sasa hivi tumebaini kwamba tunahitaji minara zaidi ya 2,500 ili kufikia maeneo yenye changamoto kubwa. Tunaamini kadiri tathmini inavyoendelea, minara itaongezeka kwa sababu kuna maeneo mengine ambayo yana minara, lakini yamepungukiwa mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu huo wa kusambaza minara ya mawasiliano nchini tunauona na Wizara inaufanyia kazi na ndiyo maana ya huu mkakati wetu wa miaka mitano kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya mawasiliano katika maeneo yote yenye matatizo makubwa ya mawasiliano. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, swali la nyongeza.

**MHE: ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kakonko, tunazo kata nne ambazo zina changamoto kubwa sana ya mawasiliano, na maeneo hayo yapo katika mpaka kati ya Tanzania na Burundi. Tunayo Kata ya Mugunzu, maeneo ya Kiniha na Nyagwijima; tunayo Kata ya Nyamtukuza maeneo ya Nyamwilonge, Lutenga na Kavungwe; tunayo Kata ya Muhangi maeneo ya Luhuru, Bwela na Nyabenge; na tunayo Kata ya Lugenge maeneo ya Kikulazo, Kasongati na Kiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba maeneo haya yanawekewa mawasiliano ili kuhakikisha usalama katika maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kwamba Jimbo la Mheshimiwa Mvano ni moja ya majimbo yaliyo kwenye maeneo ya mipaka. Katika Awamu ya Kumi na Moja ambayo tunakwenda kuitekeleza hivi karibuni, maeneo mengi yakiwemo ya kwake katika jimbo lake tutayafikia, pamoja na maeneo yote ya mpakani, maeneo ya mbuga za wanyama, na maeneo ya reli *(SGR, MGR, TAZARA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ninatambua kwamba kwenye jimbo lake kuna kata mbili kati ya alizozitaja, ambazo kwenye awamu ijayo zitapata mawasiliano. Kata zitakazobaki tutaendelea kuzihudumia kwa kadiri fedha inavyopatikana awamu kwa awamu hadi tutakavyokamilisha. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA H. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya maeneo katika Jimbo la Bagamoyo, kwa mfano eneo la Sanzale Kata ya Magomeni, eneo la Kidomole Kata ya Fukayosi na maeneo mengine yana changamoto ya kupatikana kwa mtandao, Je, Serikali ina mapango gani wa kuhakikisha kuwa

maeneo yote ya Jimbo la Bagamoyo yanapata mtandao wa uhakika kwa kuwa ni eneo la uwekezaji na eneo maalum?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunaitambua changamoto hiyo ya mawasiliano katika jimbo lake. Kwa kuwa ni eneo la uwekezaji, ni muhimu likawa na mawasiliano ya uhakika. Kwa hiyo, ninatumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* kufika katika Jimbo la Mheshimiwa Subira kufanya tathmini na kuwasilisha Wizarani ili tuangalie namna ya kutatua hiyo changamoto.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Fadhili Ngajilo, swali la nyongeza.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niulize swali la nyongeza. Bunge lililopita niliuliza swali kuhusu mawasiliano ya Iringa Mjini ambayo yana changamoto na Mheshimiwa Waziri alilijibu hapa akaagiza *TCRA* waweze kufika mara moja ndani ya Jimbo la Iringa Mjini ili kutatua changamoto hiyo. Je, ni lini wananchi wa Iringa Mjini watapata matumaini, hasa kwenye yale maeneo ambayo kuna changamoto, ikiwemo maeneo ya Nduli, Msisina, Mtalagala, Kigonzile, Mosi pamoja na Mkoga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto aliyoieleza, nimwelekeze pia Mkurugenzi Mkuu wa *USCAF*, kufika katika Jimbo la Mheshimiwa Fadhili kufanya tathmini na kutambua changamoto iliyopo ili hatua stahiki zichukuliwe. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda. Ninamwita Mheshimiwa Asha Omar Rashid, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Kutafuta Masoko ya Mwani kwa Wakulima wa Kaskazini Pemba**

**MHE. ASHA OMAR RASHID** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia masoko ya Mwani Wakulima wa Mkoa wa Kaskazini Pemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Mheshimiwa Dennis Londo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara kujibu swali Na. 12 kutoka kwa Mheshimiwa Asha Omar Rashid, Mbunge wa Viti Maalum, Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia upatikanaji wa soko la uhakika, Serikali imeweka mkakati mahsusi wa kuimarisha mnyororo wa thamani wa zao la mwani. Mkakati huo unajumuisha kufanya tafiti kuhusiana na upatikanaji wa masoko ya uhakika ya bidhaa za mwani, kuimarisha ushirikiano kati ya wakulima na wanunuzi, pamoja na kutekeleza programu za kujenga uwezo ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zinakidhi viwango na mahitaji ya masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na *TANTRADE,* tutafanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya masuala haya ya kupata masoko ya uhakika ya zao la mwani. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Omar Rashid, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA OMAR RASHID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa majibu ya Serikali. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali ina mpango upi wa kuwapatia elimu wakulima wa zao la mwani, ili waweze kulima mwani na kuvuna ama kuzalisha na uchakata zao hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, kuna mabadiliko ya mara kwa mara kwa bei ya mwani, je, Serikali ina kauli ipi ili kuwezesha kusimamia mabadiliko ya bei ya mwani na kuwaletea wakulima wa mwani kuzalisha zao hili na kuvuna na kupata bei yao iliyo nzuri, ili kuwanufaisha wakulima na wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Asha Omar Rashid Mbunge Viti Maalum Kaskazini Pemba kwa jitihada zake za kupambania zao la mwani, na pia kuwapambania wanawake ambao wanashiriki moja kwa moja katika uzalishaji na biashara ya zao la mwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira yetu ya Maendeleo ya 2020/2050 inazungumzia waziwazi kuhusiana na suala la Uchumi wa Buluu na kuimarisha mazao ya bahari. Pia, dira hii inazungumzia suala zima la kuongeza thamani ya bidhaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la elimu, Serikali imefanya jitihada kadhaa na inaendelea kufanya jitihada hizo kupitia wadau wa sekta binafsi na Serikali yenyewe. Kwa mfano, *TANTRADE* imeendelea kufanya biashara ya kuhuisha na kutangaza masoko, na pia kuimarisha wazalishaji ambao wanashiriki katika kuongeza thamani ya zao la mwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Zanzibar kuna kituo ambacho kinazalisha ama kinalea wajasiriamali, kinaitwa *Zanzibar Technology Business Incubator.* Kituo hiki kimekuwa kikitoa

mafunzo ya namna bora ya uvunaji na usindikaji, kwa maana ya kukausha na kuhifadhi, kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la mwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia wadau na taasisi kama *FAO* tumeweza kufikia vikundi 33 vya akina mama na kuwapa elimu kuhusiana na namna bora ya uvunaji, ukaushaji na uuzaji wa zao la mwani. Pamoja nao tunashirikiana na sekta binafsi kama *Seaweed Company* kule Zanzibar kwa ajili ya kuangalia namna bora ya kuwajengea uwezo vikundi ambavyo vinashiriki katika kuongeza thamani ya zao la mwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumeweza kutoa, ama kwa kupitia *FAO* tumeweza kuwajengea uwezo kwa kuwapa chanja bora kwa ajili ya kukaushia na kuwapatia maturubai kwa ajili ya kufunika mwani ili kulinda ubora wa zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na bei kutotabirika, hii inatokana na kuuza kwa kiwango kikubwa mwani ghafi. Kwa hiyo, kwa kuwa Dira ya Maendeleo 2020/2050 inatuelekeza kuongeza thamani, sasa hivi tumeweza kuona, hasa kupitia Maonesho ya Saba Saba mwani umekuwa biashara kubwa, kwa maana sasa hivi unaenda kuzalisha madawa, vipodozi, vyakula na kutoa bidhaa nyingi ambazo zinashabihiana na zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kupitia Wakala wa Stakabadhi ya Ghala *(WRB),* Wizara ya Viwanda na Biashara tumeanza kuangalia utaratibu wa kuliweka zao hili katika utaratibu wa mazao ambayo yanahitaji stakabadhi ya ghala ili kulinda bei na kumlinda mzalishaji. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asha Motto, swali la nyongeza.

**ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninaipongeza na kuishukuru sana Serikali kwa kutoa hamasa ya uzalishaji wa zao la mwani kwa wanawake wa Mkoa wa Mtwara. Zao hili limekuwa na changamoto kubwa sana ya masoko pamoja na maghala ya

kuhifadhia zao hili na kiwanda cha uchakataji wa zao hili kwa wanawake wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na changamoto hizi zinazojitokeza kwa wakulima wa zao la mwani Mkoa wa Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Motto kwa swali lake na hasa amekuwa mpambanaji mkubwa wa zao hili na mazao mengine katika Mkoa wa Mtwara, na hasa mazao ambao yana ushiriki mkubwa wa wanawake wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kwenye jibu la msingi, kupitia Dira ya Maendeleo ya 2020/2050 tunajikita kwenye kuongeza thamani ya mazao yetu likiwemo zao la mwani. Kuhusiana na bei kutotabirika, nilizungumza kwamba inatokana na kuuza mwani ghafi nje, hasa katika nchi ya Ufilipino na China na nchi nyingine za Asia, ambazo ni wadau ama ni wateja wakubwa wa zao hili. Hivyo kwa kujikita katika kuongeza thamani zao hili, kwa mpango wa kuzalisha dawa, vipodozi na vyakula vya aina mbalimbali kupitia mwani, pamoja na mwani kwenda kuorodheshwa kwenye stakabadhi za ghala, tuna uhakika kwamba unaenda *ku-stabilize* bei ya mwani na hivyo kuvutia kwa wazalishaji na washiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kupitia taasisi ya Serikali ya *TANTRADE* na mamlaka nyingine za Serikali zimeshirikiana kutafuta ama kuwapatia ithibati vikundi ambavyo vinashiriki katika uzalishaji wa zao la mwani ili wapate *certification* ambayo itawaruhusu kuuza bidhaa katika masoko ya Kimataifa. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Wakulima wa mahindi hadi sasa hivi

wamekosa soko la kuuza mahindi, takribani maeneo yote yanapolimwa hayajanunuliwa hadi sasa hivi. Je, Serikali inafanya nini kuhakikisha inapata soko la uhakika la wakulima wa mahindi ambao mpaka sasa hivi hawajauza mahindi yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa anaulizia soko la mahindi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukisisitiza kuhusiana na uzalishaji wa mazao, hasa mahindi, kwa ajili ya kuwa na hifadhi ya chakula ya uhakika. Katika kuonesha *commitment* ya Serikali tumeweza kutoa pembejeo na ruzuku mbalimbali ili mzalishaji wa mahindi apunguze gharama ya uzalishaji na hivyo kuongeza tija ya zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la soko, kwa niaba ya Serikali tumekuwa tukiendelea kuiwezesha *NFRA* (Wakala wa Hifadhi ya Chakula) kwa kumpa uwezo zaidi wa kununua mazao ya chakula. Pia tumekuwa tukitoa mikopo yenye riba nafuu kupitia Benki ya Kilimo na taasisi nyingine za fedha kwa ajili ya kuwapatia mikopo nafuu ya kununua mashine, pia kuwawezesha wanunuaji wa ndani ama kununua mahindi hayo, kuchakata unga, *ku-brand* na kuuza ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki na pia ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NFRA imewezeshwa* kwa ajili ya kuwa na vinu vikubwa vya kuhifadhi mahindi. Pia Serikali kupitia *NFRA* imekuwa ikinunua kupitia vituo vyake vya kuhifadhia mahindi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kwa hiyo, ni imani yangu na ya Serikali kwamba, suala la kununua mahindi msimu huu litaendelea kama lilivyopangwa kupitia taasisi za fedha, pia *NFRA* ambaye ni Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Ninamwita Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Ujenzi wa Mabwawa ya Umwagiliaji**

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga mabwawa ya umwagiliaji katika Kata za Mbabala, Mpunguzi, Matumbulu na Mbalawala ili vijana waweze kujihusisha na kilimo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ili kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuvutia vijana kujishughulisha na shughuli za kilimo, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imechimba visima saba. Katika kata za Matumbulu, viwili; Mbabala, viwili; Mpunguzi, viwili; na Chisichili, kimoja, Mkoani Dodoma. Visima hivyo vina uwezo wa kumwagilia eneo lenye ukubwa wa ekari 280 na kunufaisha wakulima 378.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali katika mwaka wa fedha 2026/2027 itachimba visima vitatu. Katika Kata za Mbabala, kimoja; na Mbalawala, viwili. Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kuchimba mabwawa madogo au kusimika matenki ya kuhifadhia maji yatayotumika katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji katika maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, swali la nyongeza.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; visima ambavyo vimechimbwa katika Kata za Matumbulu pamoja na Mpunguzi havijafanyiwa *pump test* na pia havijawekewa miundombinu kwa ajili ya umwagiliaji kama mabwawa. Je, ni lini

Wizara itachimba mabwawa na kuyaweka maji, ili kuwasaidia vijana katika kipindi hiki ambacho ni cha ukame?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kisima ambacho kilitakiwa kichimbwe Kata ya Mbabala katika Mtaa wa Musu hakikuchimbwa kutokana na mgogoro wa ardhi uliopo. Pia, kisima kilichochimbwa katika Mtaa wa Mapinduzi katika Kata ya Mbabala kilitoa maji kidogo sana kama vile hakukuwa na maji. Katika Mtaa wa Chisichili Kata ya Mkonze kisima kilichimbwa lakini hakikutoa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba visima hivyo upya, ili kuweka miundombinu na kusaidia vijana ambao kwa sasa hawafanyi kazi yoyote kwa sababu ya hali ngumu ya ukame ambayo inaukumba Mkoa wa Dodoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Paschal Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini kwa maswali yake mawili ya msingi. Jambo la kwanza nimthibitishie tu kwamba Serikali itafanya *pump test* na kuweka miundombinu katika maeneo yale, kwa sababu tumeshapokea *pump* za *solar* kutoka India ambazo tulikuwa tumeshaziagiza, na ipo katika utaratibu wa kuzisambaza. Kwa hiyo, tupo kwenye hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yale maeneo ambayo ameyaainisha, hususan katika nneo la Mfuso ambalo kuna kisima ambacho hakikutoa maji; Serikali, moja ya jukumu tulilonalo, kama eneo maji hayapatikani, tunachimba eneo lingine ambapo maji yanapatikana. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wananchi wa eneo husika, watuoneshe eneo lingine ili tupime na tuwachimbie kisima kingine. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Thomas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali na Wizara ya Kilimo, walituma wataalam kuja Jimbo la Katavi wakafanya *study* na upembuzi yakinifu wa Bwawa la Ipati na Bwawa la Ipwagamasigo. Je, lini Serikali itaanza miradi hii kwa sababu wananchi wa Jimbo la Katavi wanaisubiri kwa hamu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Thomas Maganga Mbunge wa Jimbo la Katavi kwa swali lake zuri la msingi. Ni kwamba, Serikali kwa sasa tupo tayari kuanza miradi hiyo ya utekelezaji mara baada ya kupokea fedha kutoka Hazina. Kwa hiyo, tupo katika huo mchakato, na baada ya hapo, wataona wakandarasi wakiingia *site*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Clayton Chipando, swali la nyongeza.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Kilimo kwa kutuletea Mradi wa Bonde la Mto Luiche ambao unaendelea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna shida kidogo ya utekelezaji wa mradi ule kwa sababu unachukua maeneo ya watu na hawajalipwa fidia. Sasa, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, hili ni ombi langu la nne ninaomba katika Bunge hili. Tafadhali, ninamwomba Waziri twende Kigoma ili nikamkutanishe na wakazi wanaomiliki maeneo ya Mto Luiche, akaongee nao wasikie kauli ya Serikali. Nimechoka kwenda kuwaelezea, wanakuwa hawanielewi tena. Ninaomba mzee wangu anisaidie.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Clayton

Chipando (Baba Levo), Mbunge wa Kigoma Mjini. Ninakiri kwamba amekuwa akinisumbua mara kwa mara kwenye simu, lakini na ofisini amefika zaidi ya mara tatu kufuatilia jambo hili. Ahadi yangu ni kufika katika lile eneo kuhakikisha kwamba tunapata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamthibitishia tu Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya Bunge hili tutaongozana mimi na yeye kuhakikisha kwamba tunakwenda kuwasikiliza wananchi na kupata ufumbuzi wa moja kwa moja katika eneo la Bonde la Mto Luiche. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Kuwalinda Wakulima Wadogo Maeneo ya Uwekezaji Miradi ya Umwagiliaji**

**MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuwalinda wakulima wadogo wenye maeneo yenye uwekezaji mkubwa wa Miradi ya Umwagiliaji Mkombozi, Pawaga-Iringa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika jitihada za kulinda maeneo ya wakulima wadogo katika skimu za umwagiliaji nchini, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa inaendelea na zoezi la kutambua, kupima na kumilikisha ardhi kwa wakulima wadogo wenye mashamba katika Skimu ya Mkombozi, yenye ukubwa wa hekta 6,000, iliyopo katika Tarafa ya Pawaga, Mkoani Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utekelezaji wake umefikia 50% na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa hatua ambazo imeendelea kuzichukua za kuanza kufanya urasimishaji. Katika zoezi la urasimishaji, je, wananchi wazawa wamepewa kipaumbele gani katika eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwalinda wakulima ni pamoja na kuhakikisha kwamba kunakuwa na masoko na bei nzuri ya mazao. Je, ni lini Serikali itaanza kununua mahindi ya wakulima? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Nancy Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa kwa maswali yake ya msingi yenye faida kwa wananchi wa mkoa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, katika yale maeneo ambayo sasa hivi tunaendelea na zoezi la kupima na kumilikisha ardhi, watu ambao wanapewa kipaumbele namba moja ni wazawa ambao walikuwa wanamiliki maeneo yale. Ndiyo maana katika zoezi hili ambalo liko chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Halmashauri ya Iringa, jambo hilo limekuwa likipewa kipaumbele na tutahakikisha wananchi wale ambao ndiyo walikuwa wazawa pale wanamiliki maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kuhusu lini *NFRA* itanunua mahindi ambayo tunakiri kwamba mwaka huu uzalishaji umekuwa mkubwa sana hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Alitutolea ufafanuzi mzuri na mimi

ninaongezea kwamba, Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Dkt. Daniel Chongolo ameshaelekeza Mamlaka ya Mazao Mchanganyiko pamoja na *CPB* kuhakikisha kwamba wanaanza kununua mazao. Hata hivyo, *NFRA* kabla ya mwisho wa mwezi Agosti, mwezi huu ambao tunauanza na wenyewe waingie sokoni kuongeza nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelekezo hayo, ninatoa rai kwa wananchi. Tumeshasikia taarifa zimetolewa na mamlaka za hali ya hewa nchini pamoja na duniani, kuhusu uwepo au utabiri wa mvua za *El Nino* katika mwaka huu. Maana yake, kama kukiwa na *El Nino* maana yake kutakuwa na changamoto katika uzalishaji. Kama kutakuwa na changamoto katika uzalishaji, maana yake tunaweza kuwa na hatari kubwa ya janga la njaa katika mwaka unaofuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninatoa rai kwa wananchi wote kuhakikisha kwanza tutunze chakula ambacho tumekivuna mwaka huu kwa ajili ya mwakani, wakati huo huo *NFRA* watakapokuja, maana yake kumekuwa na tabia ya wananchi kuuza chakula chote na mwisho kuja kulalamika kwa ajili ya kutaka kupewa chakula cha msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, rai ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatunza chakula tulichokipata. Yaani tuhakikishe kwamba tunakuwa na chakula cha kukaa nacho kwa miaka miwili kabla ya kufikiria kwenda kukiuza ili kupata fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa hiyo, hiyo niliona iwe ni rai yetu ya kwanza kabla ya kufikiria kwenda kuyauza mazao yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wakulima wa chai Wilaya ya Rungwe wanatia huruma kweli kweli. Je, ni lini Serikali itawapa furaha wakulima wa chai wa Wilaya ya Rungwe kwa kufungua viwanda ambavyo vilifungwa kwa muda mrefu, Kiwanda cha *WATCO* kilichopo Katumba na Kiwanda cha Chivanje? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya kwa swali lake zuri sana na la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunafahamu kuna changamoto kubwa katika sekta ya chai. Wizara ya Kilimo kupitia Waziri *Comrade* Mheshimiwa Dkt. Daniel Chongolo, tumeshafanya kikao na wadau wa chai na Wabunge wanaotokea katika maeneo yanayozalisha chai na tuna mkakati wa pamoja wa kuhakikisha kwamba tunaliokoa zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamthibitishia tu kwamba, tuko kwenye hatua nzuri ya kuzungumza na wamiliki wa maeneo yale pamoja na zile benki ambazo ziliwakopesha wale wanaomiliki vile viwanda, ili kupata namna bora ya kuwaondoa wakulima wa chai katika ile changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kuna hatua ambazo tumeshazifikia na ninafikiri katika wiki moja kuanzia sasa, Waziri wa Kilimo atakuja na kuzitangaza katika maeneo yale ambayo wakulima wa chai wanapata. Kwa hiyo, waondoe shaka tu wakulima kwamba, tuna hatua nzuri na tutalimaliza jambo hili kama ambavyo tulikuwa tumekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza ninaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutupa mradi wa kujengewa bwawa la umwagiliaji la thamani ya shilingi 76,000,000,000 katika Kata ya Bashay ambayo itakwenda kuhudumia Skimu ya Bashay na Dirim.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bwawa hili litakwenda kuathiri mashamba na nyumba za wananchi wa karibu vitongoji viwili. Je, nini mpango wa Serikali kuhusu fidia kwa wananchi hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Emanuel, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza ni kwamba, karibu katika maeneo mengi ambayo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inafanya miradi ile ni kwa faida ya wananchi wenyewe. Ndiyo maana wamiliki wa ile miradi wanabaki kuwa wao wenyewe, isipokuwa tu sisi kama Tume tunakuwa na jukumu la usimamizi, uratibu na matengenezo baada ya kukamilisha ile miundombinu katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, linapofika suala la fidia maana yake mara nyingi Tume imekuwa haijihusishi 100% kwa sababu mradi ule unakuwa ni mali ya wananchi, isipokuwa tu katika maeneo ambayo tutaona kuna uhitaji wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, jambo hili tumekuwa tukishirikiana pamoja na halmashauri. Tutafika vilevile katika eneo la Mbunge ili tuweze kupata ufumbuzi wa kudumu wa kuhakikisha kwamba mradi ule wa thamani ya shilingi 76,000,000,000 katika eneo la Bashay unawanufaisha wananchi wale. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, sasa ninamwita Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, Mbunge wa Mpanda Mjini, aulize swali lake.

Na. 15

**Kupunguza Riba za Mikopo ya Biashara kwenye Mabenki**

**MHE. HAIDARY H. SUMRY** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza riba za mikopo ya biashara katika mabenki ili kuwawezesha wafanyabiashara kulipa mikopo yao kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali haliingilii moja kwa moja upangaji wa viwango vya riba za mikopo katika benki za biashara zinazofanya shughuli zake hapa nchini. Aidha, viwango vya riba katika benki hizo huamuliwa kwa kuzingatia misingi ya soko, ikiwemo viwango vya mfumuko wa bei, vihatarishi vya mikopo kutolipwa, gharama za uendeshaji wa benki husika pamoja na kiwango cha faida kinacholenga kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisheria na za kiusimamizi na kuwezesha benki za biashara kutoa mikopo kwa riba nafuu zaidi, ikiwemo kuendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kudhibiti mfumuko wa bei, ambao ni moja ya kiashiria muhimu kinachotumika katika kukokotoa na kuamua riba inayotozwa kwenye mikopo na benki hizi za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha azma hiyo, Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kufanya mabadiliko katika viwango vya riba vya Benki Kuu (*Central Bank Rate)* kuendana na mwelekeo wa kiuchumi, ili kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei

unabaki ndani ya wigo, huku ikiendelea kuhakikisha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye uchumi, ili kuchagiza upatikanaji wa mikopo kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha mfumo wa ulinganishi wa bei unaojulikana kama *Price Comparator System*. Mfumo huu unaongeza uwazi kuhusu viwango vya riba na gharama zinazotozwa na taasisi mbalimbali za kifedha, hivyo, kuwasaidia wakopaji kufanya maamuzi sahihi kuhusu huduma za mikopo wanazozihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu vilevile unachochea ushindani miongoni mwa benki za kibiashara, jambo linaloweza kuchangia kupungua kwa gharama za mikopo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea kuhimiza benki na taasisi za fedha kutumia kanzidata ya taarifa za wakopaji *(Credit Reference Bureau),* ambayo hutoa taarifa za kihistoria za ukopaji na ulipaji wa madeni ya wakopaji. Mfumo huu hupunguza wasiwasi wa benki kuhusu vihatarishi vya mikopo kutokulipwa, hivyo kusaidia kupunguza gharama za tathmini ya mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, swali la nyongeza.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni kuziachia benki kupanga zenyewe hizi riba za mikopo, kwamba inaweza ikapelekea wafanyabiashara kuumia kwa kupewa riba ambazo siyo rafiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kumekuwepo pia, pamoja na changamoto nyingi, lakini pia sababu nyingine ambayo inapelekea riba hizi kuwa kubwa ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania kutoza riba kubwa kwenye mikopo ambayo inatoa kwenye hizi taasisi za fedha. Je, ni lini Benki Kuu ya Tanzania itapunguza riba kwenye mikopo yake, ili kuzifanya hizi taasisi za

fedha ziweze kuwahudumia vizuri wananchi wetu, wafanyabiashara wa nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kupata nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, Mbunge wa Mpanda Mjini kwa kuendelea kuwasemea wananchi wake na wafanyabiashara wa Jimbo la Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Haidary Sumry, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikianza na swali la kwanza, hili kwanza niseme ya kwamba kama Serikali haijaachia benki kuweza kuamua kwamba zitoze riba kiasi gani. Isipokuwa kama nilivyosema kwenye jawabu langu la msingi ni kwamba, riba hizi huamuliwa na misingi ya soko. Misingi ya soko hii kuna sababu mbalimbali, ikiwemo mfumuko wa bei kama nilivyokwisha kutahadharisha pamoja na vihatarishi vya mikopo pamoja na gharama za kuendesha benki zenyewe, benki husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali haiko mbali kuhakikisha kwamba inaratibu riba hizi kupitia Benki Kuu yetu ya Tanzania. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, Benki Kuu ya Tanzania imekuja na Mfumo wa Ulinganishi wa Bei unaoitwa *Price Comparator System*, ambapo mfumo huu kwanza, unamwezesha mkopaji kuwa na uwazi wa kupata huduma ya mikopo anayohitaji. Pia, unachochea ushindani wa benki hizi ambazo mwisho wa siku utachochea kupunguza gharama na riba za mkopo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, mfumo huu unaongeza uwazi wa viwango vya riba kama ambavyo nimesema kwenye jibu langu la msingi na hili linawekwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa mwaka 2020, vile vihatarishi vya mikopo kutokulipwa tulikuwa kwenye 12%, lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumzia kwa taarifa za mpaka mwezi Juni, tuko kwenye asilimia 2.6. Hii inamaanisha ya kwamba, Serikali imeratibu vizuri kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hawa wanapata mikopo ya riba nafuu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili ambapo Mheshimiwa anataka kujua kwamba Serikali ina maoni gani kuhusu kutaka kupunguza riba ambayo inaendelea kutolewa na benki?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni uhalisia kabisa kwamba, tangu mwaka 2020 ambapo *COVID-19* ilipoingia nchini, vita ya Ukraine na vita nyingine ambayo inaendelea mpaka sasa hivi Mashariki ya Kati, ni dhahiri kwamba nchi nyingi ukiangalia ile *commercial lending rate*, kwa maana ya wastani wa riba za kibiashara imeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunavyozungumza sasa hivi, Nchi yetu ya Tanzania kwa maana ya *commercial lending rate* ina-*range* kuanzia 11.9% mpaka 16.3%. Hii ni riba nafuu, lakini kama Serikali bado tunaendelea kuratibu na kuongea na wadau wetu kupitia Benki Kuu ya Tanzania kuhakikisha kwamba riba hizi zilizopo sasa hivi zinapunguzwa ili kuwaletea nafuu wafanyabiashara wetu na kuhakikisha kwamba, tunapata wafanyabiashara wengi na uchumi wa nchi yetu ya Tanzania unaendelea kuimarika na kukua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, swali la nyongeza.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa. Tarehe 2 Julai, Kamati ya Sera ya Fedha *(MPC)* ilitoa tamko la kuongeza riba kutoka asilimia 5.75 kwenda asilimia 6.25. Madhara yake ni kwamba, benki za kibiashara zitaenda kupandisha riba kwa sekta binafsi na madhara yake ni kwamba, utekelezaji wa bajeti ya 2026/2027 utaenda kuathirika

kidogo kwa kuwa sekta binafsi inategemewa kwa 70%. Je, ipi kauli ya Serikali ili iweze kupunguza riba hiyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mbunge mwenzangu kwa swali lake zuri, lakini pia linalolenga kuleta unafuu wa riba kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha ninasema wazi; kwanza kama nilivyosema kwenye jawabu langu la msingi, Serikali imedhamiria kabisa kwa 100% kuhakikisha kwamba hii mikopo ya kibiashara ambayo inatolewa kwa sasa hivi, ambayo ina-*range* kuanzia 16% – 20%, kupitia Benki Kuu yetu ya Tanzania, kupitia mfumo huu wa *Price Comparator System* ambao unaweka uwazi wa riba hizi, sisi kama Serikali tumedhamiria kuhakikisha kwamba, tunakaa na wenzetu wa benki za kibiashara kuona namna ambavyo tunapunguza riba hizi ili kutengeneza wafanyabiashara wengi zaidi ambao wataongeza uchumi wetu kulingana na Dira yetu ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simai Said, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI MOHAMMED SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Serikali inakuja katika Bunge lako Tukufu katika kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali. Ni utaratibu upi Serikali inatumia katika kupima au kujua ni vipaumbele gani wafanyabiashara wanapata katika kuwapatia mikopo ndani ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pia tumepakana na nchi nane kama tutachukua pamoja na *Comoros* itakuwa ya tisa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali la nyongeza ni moja. Haya Mheshimiwa jibu swali la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamsikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Hajasikia swali la nyongeza hilo la kwanza. Ni vigezo gani vinatumika kwenye…

**MHE. SIMAI MOHAMMED SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu upi Serikali inatumia tunapokuja kila mwaka hapa katika kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali, ili na sisi Wabunge pia tujue? Kwa mfano, kila mwaka Serikali inakuja Bungeni katika kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali na sisi Wabunge tunataka tuunge mkono vipaumbele vya Serikali. Ni utaratibu upi Serikali inatumia katika kupima jinsi gani hii mikopo tunaweza kuwapatia wafanyabiashara katika maeneo tofauti ndani ya Tanzania? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, nimwombe na nikiombe Kiti chako kama itampendeza Mheshimiwa Mbunge alilete swali hili kama swali la msingi na sisi kama Wizara ya Fedha tutalipatia majibu ya kutosha na toshelezi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana.

Tunakwenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ninamwita Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima, Mbunge wa Newala Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Hitaji la Josho - Newala Mjini**

**MHE. RASHID M. MTIMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga josho la kuogeshea mifugo katika Jimbo la Newala Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima, Mbunge wa Newala Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi na ukarabati wa majosho katika kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na Kupe na Mbung'o nchini. Katika kutekeleza azma hiyo Serikali ilianza kutekeleza mpango wa ujenzi wa majosho tangu mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo hadi sasa jumla ya majosho 754 yamejengwa nchini kwa thamani ya shilingi bilioni 15.19.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imejielekeza katika kutekeleza na kukamilisha miradi ya kimkakati ikiwemo kuendelea na mpango wa chanjo na utambuzi wa mifugo nchi nzima kwa lengo la kufikia azma ya kutokomeza magonjwa yenye athari kwa afya za wanyama na binadamu nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuratibu ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa miundombinu muhimu ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ikiwemo majosho ya Newala Mjini, kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za mifugo kwa wananchi kadri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, ninatoa rai kwa Halmashauri ya Newala Mjini, kutenga fedha kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majosho katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya kwenye sekta hii na kuweza kujenga majosho 754. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Wizara katika swali langu lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Wizara ipo tayari kufuatilia utekelezaji wa rai iliyoitoa kwenye majibu haya ikiwemo Mheshimiwa Waziri kufanya ziara Jimbo la Newala Mjini ili kujionea namna ya kutekeleza rai hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, kwa kuwa Serikali imesema kwamba kwa sasa kipaumbele ni kutoa chanjo kwa mifugo, ni mpango upi sasa upo kwa mwaka huu 2026/2027 wa kutoa chanjo ya mifugo katika Jimbo la Newala Mjini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima kwa juhudi zake nyingi za kufuatilia afya ya mifugo iliyopo katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza; ninaamini tangu Mheshimiwa Waziri amekabidhiwa nafasi hiyo ya kusimamia sekta hii ya mifugo na uvuvi amekwishafanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo ninajua atakuwa tayari kabisa kuambatana na Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake ili kuangalia changamoto za wafugaji waliopo katika eneo lake kadri ratiba zitakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 tulitenga bajeti ya kiasi cha shilingi bilioni 62.2 na fedha hizo zimetumika vizuri na tuliweza kukamilisha uchanjaji wa 66.2% ya mifugo yote tuliyokuwa tumepanga kuichanja kwa mwaka huo. Kwa mwaka huu wa fedha tumetenga fedha shilingi bilioni 30.8 ambayo tutaitumia na tayari tumekwishaanza utaratibu wa manunuzi ambao unaelekea kukamilika ili tuanze zoezi hili kwa wakati bila kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Jimbo lake la Newala Mjini litakuwa ni kati ya majimbo

ambayo pia utaratibu huu wa uchanjaji na utambuzi wa mifugo utaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunahamia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninamwita Mheshimiwa Mohammed Kassim Salum, Mbunge wa Mpendae, sasa aulize swali lake.

Na. 17

**Kuwapatia Polisi Vitendea Kazi vya Kisasa**

**MHE. MOHAMMED KASSIM SALUM** aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuhakikisha Polisi wote nchini wanakuwa na vitendea kazi kama *Radio Calls* na kompyuta ili kurahisisha mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Kassim Salum, Mbunge wa Mpendae, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango wa vyombo vya ulinzi na usalama katika kudumisha amani na utulivu nchini. Serikali imeendelea kuliwezesha Jeshi la Polisi kwa vifaa vya kisasa kupitia bajeti kuu. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Jeshi la Polisi limetengewa jumla ya shilingi 155,952,240,241 kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya Jeshi ambapo shilingi 30,006,499,000 zitagharamia ununuzi wa magari kwa ajili ya operesheni mbalimbali za kipolisi; na shilingi 6,000,000,000 zitagharamia ununuzi wa pikipiki kwa ajili ya Jeshi la Polisi katika ngazi ya Kata na Shehia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia shilingi 91,735,559,000.71 zitagharamia ununuzi wa vifaa vya kijeshi; shilingi 14,368,723,590 zitagharamia usimikaji wa mifumo ya TEHAMA na ununuzi wa *Radio Calls* za masafa marefu; na shilingi bilioni 1.8 zitagharamia ununuzi na usimikaji wa minara 15 ya mawasiliano ya *Radio Call* ya masafa mafupi. Vitendea kazi hivi vitasaidia utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi kwa weledi na ufanisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohammed Kassim Salum, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMMED KASSIM SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ni lini Serikali itahimiza maboresho ya vifaa hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Kassim Salum, Mbunge wa Jimbo la Mpendae, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, tayari fedha hizi zilikwisha kutengwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, lakini kwa mwaka huu wa fedha, pia tumepata mgawanyo huu wa fedha tunatarajia kupata kutoka Hazina na mara baada ya tutakapopokea fedha hizi tutaanza kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shadya Haji Omar, swali la nyongeza.

**MHE. SHADYA HAJI OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tumekuwa tukiona na bado tunashuhudia upotevu wa watoto hata pale wazazi wao wanapokuwa wanakimbilia katika vituo vya Polisi ambavyo vipo karibu na wao kwa ajili ya kupata usaidizi wa kuwapata watoto hawa na bado inaonekana kuna ugumu

wa kupata taarifa hizi kwa haraka ili kwenda kuokoa watoto wao sehemu ambazo wamepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mfumo maalum wa kuviunganisha vituo hivi vya Polisi ambavyo vitawasaidia wananchi kupata taarifa za walipopatikana watoto wao kwa haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Shadya Haji Omar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna nyakati ambazo kunatokea taarifa za upotevu wa watoto, lakini hata pia inapotokea taarifa ya upotevu wa mali. Jeshi la Polisi wakati wote limekuwa likifanya upelelezi kwa kutumia ushirikiano mzuri unaopewa na wananchi, lakini pia kufanya utaratibu wa kufanya upelelezi kwa mujibu wa mbinu za kimedani walizonazo ili kuweza kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapatikana pale ambapo taarifa hizo zinatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimekuwa zikitokea mara moja moja na inategemeana na mazingira ambayo mtoto ameweza kupotea. Katika utaratibu huo ninadhani jambo la msingi hapa ni kuhamasisha na kusisitiza wananchi na ni rai yangu kwa wananchi wote, lakini pia wazazi kuwa makini na watoto katika maeneo ya elimu, lakini pia katika maeneo ambayo watoto wanakwenda ikiwa kwenye maeneo ya michezo na maeneo mengine yoyote kuhakikisha mzazi anatekeleza wajibu wake wa kwanza wa kuhakikisha kwamba ana-*provide* ile *parental care* kuhakikisha mtoto wakati wote unajua na una taarifa za alipo ili hata inapotokea upotevu uweze kulisaidia Jeshi la Polisi kwa haraka sana kupata taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ipo mifumo ambayo inatumika ya kisasa kwenye nchi zilizoendelea na Jeshi la Polisi linaingia katika mifumo ya kupata *camera* kwenye maeneo yote na kutengeneza zile *security system* ambazo zinaweza zikasaidia

*tracking* pale mtoto au mali ama mtu mzima pale inapotokea kwamba amepata changamoto za kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize tu kwamba jukumu la ulinzi na usalama wa raia na mali zao lakini pia watoto kama alivyosema ni la kwetu sisi sote na Jeshi la Polisi linakuja kutekeleza wajibu wa kisheria wa kusimamia haki hizo, lakini pia kuhakikisha kwamba watu wote wanakuwa salama. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Imamu Mtumwa Vuai, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

Na. 18

**Kuimarisha Idara ya Uhamiaji katika Matumizi ya Teknolojia za Kisasa**

**MHE. IMAMU MTUMWA VUAI** aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuimarisha Idara ya Uhamiaji kutumia teknolojia za kisasa za utambuzi na udhibiti wa mipaka ili kuimarisha usalama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Imamu Mtumwa Vuai, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya Uhamiaji kwa teknolojia ya kisasa kwa kuboresha mtandao na kujenga mifumo mipya na kuendelea kuimarisha mifumo iliyopo ambapo maboresho hayo yanajumuisha uanzishaji wa Mfumo wa *Advance Passenger Information*, *Passenger Name Record*, uboreshaji wa mfumo wa *e-Border Management* Control, *Immigration Common Gateway Interface*, pamoja na maboresho ya miundombinu ya vituo vya kuhifadhi mifumo ya Serikali ili

kuongeza usalama, upatikanaji na mwendelezo wa huduma za Uhamiaji Mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa matumizi ya mifumo ya kiteknolojia umerahisisha sana utolewaji wa huduma za kiuhamiaji sambamba na kuimarisha usalama wa nchi hasa katika utambuzi na udhibiti wa mipaka. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilitoa kiasi cha fedha shilingi 69,000,000,000 kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa vifaa vya mifumo ya Uhamiaji Mtandao, kukarabati miundombinu ya majengo ya vituo ili mifumo hiyo iweze kusimikwa, kuongeza uwezo wa vifaa vya kuhifadhi *data* na kuendesha mifumo katika kituo kikuu cha kuhifadhi mifumo na *data* zilizozalishwa *(National Internet Data Centre)* kilichoko Dar es Salaam na kituo cha kujikinga na majanga *(Disaster Recovery site)* kilichoko Mazizini, Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Imamu Mtumwa Vuai, swali la nyongeza.

**MHE. IMAMU MTUMWA VUAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa baadhi ya wageni huingia kihalali, lakini baadaye huzidisha muda wa vibali vyao. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia teknolojia kuwabaini na kuwafuatilia moja kwa moja kabla hawajawa wahamiaji haramu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kutokana na ongezeko kubwa la wageni wanaoingia Zanzibar ni lini tutakuwa na mfumo wa *biometric* unaowezesha msafiri kuhakikiwa na kupita uhamiaji kwa haraka bila kupunguza kiwango cha usalama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Imamu Mtumwa Vuai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni kweli kwamba tunapokea wageni na wanaingia ndani ya nchi kupitia *border* zetu au maeneo na mipaka ambayo tunayo lakini pia viwanja vyetu vya ndege. Kupitia Idara yetu ya Uhamiaji tunao mfumo wa *Internal border* ambao unatusaidia kutambua taarifa zao. Pale anapoingia ndani ya nchi tunafahamu kama ana miezi mitatu ya kuishi hapa nchini na muda wake unapofikia mwisho tunapata taarifa kupitia mifumo na kuanza kufanya utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa awali ambao upo ambao tulikuwa tunaendelea kuutekeleza na sasa tunaingia katika utaratibu wa mifumo. Moja, tulikuwa tunahakikisha tunafanya doria; Mbili, tunafanya *patrol;* na Tatu, zote hizi ilikuwa inasaidia kufanya misako ili kuweza kutambua wale walio *overstay* hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kila miezi mitatu pia tulikuwa tunafanya zoezi hilo, lakini katika kila kipindi cha miezi sita pia tumekuwa na operesheni maalum ya kuwasaka hao wahamiaji ambao wamezidisha muda ambao walikuja kwa utaratibu, lakini muda wao wa kuishi nchini umezidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mifumo ambayo tunaenda kuiweka itakuwa inatoa meseji kwa mtu anapozidisha muda, lakini pia kuweza kutambua *movement* zao ndani. Mipango hiyo tayari tumekwishaanza kwa kufanya usimikaji wa mifumo na maboresho ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatupatia fedha kwenye mwaka wa fedha huu wa bajeti ambapo tunaendelea kuiimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pili la swali lake amezungumzia upande wa Zanzibar kuhusu wageni wanaoingia kama wanaingia kwa wingi, ni namna gani ambavyo tunaweza tukawasaidia waweze kupita kwa haraka. Mifumo tunayo tayari, tunayo *JNIA* hapo Uwanja wa Julius Kambarage Nyerere, lakini pia Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro pamoja na Uwanja wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mfumo wetu wa *APIS* ambao tayari tumefanya *installation* kwenye hayo maeneo, ambao

unatusaidia kuhakikisha kwamba abiria anaweza kuingiza taarifa zake hata akiwa nyumbani kama hana haja ya kuja kuonana na Afisa wa Uhamiaji. Mfumo mwingine ambao umefungwa ni wa *eye contact* ambapo anafika na kuweka mfumo wake wa sura na taarifa zake zote zikapita na akafunguliwa akapita bila kuhangaika kumwona Afisa wa Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vioski vingi ambavyo tumevifungua sasa na tunaendelea kufungua kwenye viwanja vya ndege na kwenye maeneo ya bandari na maeneo mengine ambayo ni rasmi, lakini tuna mfumo pia wa *electronic gates* ambazo ninadhani Wabunge wamekwishaona katika Uwanja wa Julius Kambarage Nyerere na Kilimanjaro na pia pale Zanzibar ambapo unakuja na *passport* yako na una-*scan* na baada ya hapo unapita na unahudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lililopo ni kuongeza idadi ili abiria wetu au wateja wanaokuja waweze kuhudumiwa kwa haraka. Hata hivyo taarifa njema ni kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwishatupatia fedha na tumeweza kufanya *installation* ya mifumo mbalimbali kwenye vituo 22, kwenye balozi zetu zote nje ya nchi 47, lakini pia katika Ofisi za Uhamiaji zaidi ya 31 tumefanya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hata *visa* zinaweza zikapatikana kupitia balozi zetu huko nje na ukapata *electronic visa* bila kufika hapa, hii yote imeendelea kuongeza ufanisi katika Idara ya Uhamiaji na kuhakikisha wageni wanakuja kwa haraka na wanahudumiwa kwa haraka pia ili kusiwe na usumbufu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninaomba niwaletee matangazo tuliyonayo hapa mezani. Kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Spika kutoka Jijini Dar es Salaam; ndugu Joanitha Mrengwa ambaye ni Rais wa *Female*

*Future Cohort 12*; ndugu Suzanne Ndomba, Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania; na ndugu Joyce Nangai, Mratibu wa *Female Future Programme*, Chama cha Waajiri Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 105 wa Mheshimiwa Spika, ambao ni wajumbe washiriki wa *Programme ya Female Future Cohort 12* kutoka Chama cha Waajiri Tanzania. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Salum Khamis Salum, ambao ni watumishi kutoka Halmashauri ya Meatu, Mkoani Simiyu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, ndugu zake kutoka Katama Tandahimba, Mkoani Mtwara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ambao ni viongozi wa dini kutoka Mbozi, Mkoani Songwe. Karibuni sana viongozi wetu wa dini. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaye ndugu Gabriel Msulwa kutoka Mkoani Tabora; ndugu Hemed Mayenya, Mjasiriamali kutoka Mkoani Morogoro; na ndugu Kenedy Mwasaba, mwanafunzi wa Ndaki ya Tiba kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Maafisa sita wa Kampuni ya *iCare Technology* wauzaji na wasambazaji wa vifaa vya *IT* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 21 wanaosoma Kozi ya Udaktari kutoka Chuo Kikuu cha Kairuki, *Campus* ya Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa Benki ya Watu wa Zanzibar *(The People's Bank of Zanzibar Limited)*

imefungua rasmi tawi lake jipya hapa Bungeni na limeanza kutoa huduma zote za kibenki. *(Makofi)*

Lengo ni kuhakikisha wateja wa Benki hiyo wanapata huduma kwa urahisi na ufanisi bila kuathiri majukumu yao. Waheshimiwa Wabunge wote na Watumishi wa Bunge mnakaribishwa kutembelea tawi hili ili muweze kupata huduma za kibenki karibu na maeneo yenu ya kazi.

Tangazo kutoka Ofisi ya Katibu wetu wa Bunge: Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa kikao cha Kamati ya Uongozi kitafanyika leo siku ya Jumatano tarehe 26 Agosti, 2026, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Kikao hiki kitafanyika katika Ukumbi wa Spika, ghorofa ya kwanza Jengo la Utawala. Aidha, mnajulishwa kuwa kikao cha *briefing* kwa Wabunge wote kilichopangwa kufanyika leo saa 10 jioni kimeahirishwa hadi mtakapotaarifiwa kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Tangazo lingine, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Bunge imeandaa Tamasha la Michezo na Burudani (Bunge Bonanza) kwa udhamini wa *NMB* ambalo linatarajiwa kufanyika siku ya Jumamosi tarehe 29 Agosti, 2026 katika Viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlini hapa Dodoma, kauli mbiu ya Bonanza hilo ni "Pamoja *AFCON* 2027 Tanzania Tupo Tayari".

Bonanza hili litawashirikisha Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, Wizara na Taasisi za Umma, Vyuo Vikuu vilivyopo Dodoma na Vilabu vya mazoezi Dodoma. Bonanza hili litatanguliwa na matembezi yatakayoanzia Chuo cha Mipango saa 12.00 asubuhi kuelekea Uwanja wa John Merlini.

Baadhi ya michezo ya ushindani na burudani itakayofanyika ni pamoja na Mpira wa Miguu, Mpira wa Pete, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Wavu, Mbio, Kuvuta Kamba, Kukimbiza Kuku, Drafti, Karata, Kupita kwenye Pipa na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge wote na Watumishi wa Bunge mnahimizwa kushiriki Bonanza hili muhimu. Hili ni tangazo kutoka Ofisi ya Katibu wetu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 5.40 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 27 Agosti, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA